**DED** akiri ubadhirifu, aomba radhi Baraza la Madiwani

UKURASA 16



**MZEE** Mwinyi aeleza alivyoupata urais wa Tanzania kwa bahati

UKURASA 4


SAFARI YA MAISHA
Inavyoakisi kuibuka upya mageuzi kiuchumi, kisiasa
Ukurasa 12
Ukurasa 13
Ushirikiano na Kenya usiangalie kingine ila maslahi ya Tanzania
siasa
JUMATANO MEI 12, 2021
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe
MELES ZENAWI:
Ukurasa 14
Muasi hadi Waziri Mkuu, aliacha shule kumwangusha Mengistu
Ahadi uteuzi usiojali itikadi
Na Sabato Kasika
• Wadau wataka uanzishwe na katiba mpya
• Wahofia usilenge kuangamiza wapinzani

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Mei 12, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

...A WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580578

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ

...0745 700710


# Dawa rasmi corona hizi

**WAZIRI** Mulamula aipa neno WHO kuhusu chanjo...Endelea Ukurasa 2, 19



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**PM AZIBANA TAASISI KULIPA ANKARA MAJI**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameagiza taasisi za serikali zinazodaiwa ankra za maji kulipa fedha hizo kwa kuwa imebainika kuna madeni...

UKURASA WA 4

**CHANZO FOLENI MALORI BANDARINI CHATAJWA**

MKURUGENZI wa Bandari ya Dar es Salaam, Elihuruma Lema, amesema kutumika kwa mfumo wa kidijitali katika bandari hiyo ni mojawapo ya...

UKURASA WA 4

**DPP AKOSOLEWA KUKUSANYA FEDHA ZA UHUJUMU UCHUMI**

WAKILI wa kujitegemea, Peter Madeleka, amesema Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) hapaswi kukusanya fedha za makosa ya uhujumu uchumi kwa mujibu...


# DPP Biswalo ateuliwa kuwa jaji

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati) akimkabidhi cheti Mhazini Mkuu wa Benki ya NMB, Azizi Chacha, kwa kutambua mchango wa NMB katika kufanikisha mashindano ya kitaifa ya Ubunifu, Sayansi na Teknolojia (MAKISATU 2021) yaliyofanyika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. Kulia ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Rais Samia mgeni rasmi Baraza la Eid

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA HAZIKWEPANI** UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK. 6

# Dawa rasmi za corona hizi

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

SERIKALI imesema dawa za asili 23 zimeidhinishwa baada ya kupimwa na maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapambano dhidi ya corona.

Aidha, wabunge wametaka tahadhara kubwa kuchukuliwa katika kuchagua chanjo ya kutumika nchini katika kukabili ugonjwa huo.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2021/22.

"Serikali inaendelea kufanya utafiti wa kina wa kitaalamu wa dawa mbalimbali zinazotumika katika kipindi cha mapambano dhidi ya COVID-19," alisema.

Alizitaja dawa hizo ni NIMR-CAF, Mashimo Hero, Lishe, Dawa ya Asili, COVORANXA, BINGWA, MGENDELANDAA, NUT, TULSI PUS, NIGELLA SATIRAT, NIGELLA PLUS, COVIDOL, PL JILAMBE Lemon Juice, Shentembo Herbal, Shekilindi, OLARAMI.

Nyingine ni Tiga Tiga, BYCARO, Mtihaki Mtemi, Planet++, BUPIJI, UZIMA HERBAL DROPS.

"Pamoja na matumizi ya dawa za kunywa, dawa za kujifukiza zilizotumika kwa wingi baada ya uhamasishaji mkubwa na utengenezaji wa mafuta tete zilizozalishwa na taasisi za SIDO-DSM, Vingunguti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma," alisema.

"Kupitia taasisi ya NIMR serikali inaendelea kuzifanyia utafiti wa kina wa kitaalamu dawa mbalimbali zilizotumika katika kipindi cha mapambano didi ya COVID-19," alisema.

Waziri Gwajima alisma serikali imeendelea kupambana na corona kwa kutoa miongozo 15 ya namna ya kuchukua tahadhari kwa kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka ya sabuni, kutumia vipukusi, kufanya mazoezi, lishe bora na kuvaa barakoa.

**ANGALIZO KWA CHANJO**

Akichangia mjadala huo, Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima, aliishauri serikali kuwa makini na chanjo ya corona kwa kuwa hadi sasa hakuna uthibitisho wa kisayansi kwa mashirika yanayohusika duniani juu ya madhara yatokanayo na chanjo hizo.

Alisema ni muhimu sana serikali kusubiri kabla ya kufanya uamuzi kwa kuwa bado kuna madhara mngi yanayotajwa kwa chanjo zilizokwishaanza kutumika duniani.

Alisema hana pingazi dhidi ya chanjo yoyote kwa kuwa nchi imesharuhusu matumizi ya chanjo nyingine za magonjwa mengine bila pingamizi.

Kwa mujibu wa Gwajima, kuna tafiti nyingi zinaendela duniani kwa chanjo, na kwamba ya corona imekuwa tofauti na nyingine kwa kuwa kinachofanyika ni kupunguza nguvu ya virusi hivyo vinavyoingizwa kwenye mwili wa mtu, na kinga ya mwili zikichukua hatau kinga inatengenezwa na mwili kupambana na kirusi au ugonjwa.

"Chanjo ya corona ni ya mwendo kasi, miezi mitatu minne tayari, unapojaribu kuliza hii kwanini haraka, kuna magonjwa ya malaria na mengine amabyo tungetegemea mfanye haraka ili watu waokolewe, sababu wanayotoa ni kuongezeka kwa tekonolojia, rasilimali kutoka makampuni mengi na ugonjwa wa mlipuko," alisema.

Gwajima alisema chanjo ya corona ni MRA maana yake ni aina wanayochukua utu wa mtu, na kwamba suala la utu wa mtu na binadamu atakayezaliwa baada ya miaka sita kuendelea atakuwa wa aina gani.




Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maonyesho ya 45 ya biashara ya kimataifa yatakayoanza Juni 28 hadi Julai 13 mwaka huu, viwanja vya Julius Nyerere Barabara ya Kilwa. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE), Edwin Rutageruka. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# PM azibana taasisi ankara za maji

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza taasisi za serikali zinazodaiwa ankra za maji kulipa fedha hizo kwa kuwa imebainika kuna madeni mengi zinadaiwa na Wizara ya Maji.

Aidha, amemtaka Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Anthony Sanga, atoe taarifa ya taasisi ambazo hazidaiwi ili zilipe fedha hiyo kwa wakati na isaidie kwenye utekelezaji wa miradi ya maji.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizindua ripoti ya tathmini ya utendaji kazi kwa mamlaka za maji nchini iliyoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) na vitabu vya mwongozo wa uandaaji wa miradi ya maji kwa Wizara ya Maji.

"Mamlaka zihakikishe wanaotumia maji wanalipa ankra zao kwa wakati zikiwemo taasisi za serikali tumeona madeni mengi kwenye Wizara ya Maji wakizidai taasisi nyingine za serikali na wao wanadhani kwa kuwa ni taasisi za serikali hawapaswi kulipa ankra za maji, kila mtumia maji anapaswa kulipa ankra," alisema.

Alisema hakuna sera ya biashara lakini huo ni mchango wa kufanya maboresho katika miradi ya maji.

"Hatufanyi biashara lakini ule ni mchango wa kuwezesha kufanya maboresho ya miradi yetu, kununua vipuli lakini na kuwezesha mamlaka kufanya kazi kwa ufanisi, Katibu Mkuu kwa nyakati tofauti toa taarifa kwa waziri wako ukionyesha ni taasisi zipi hazilipi bili ili zilipe," alisema.

Majaliwa aliitaka EWURA kukaa na kuangalia ankara za maji ili huduma hiyo ipatikane kwa bei nafuu kwa wananchi hivyo kupunguza malalamiko yasiyo na lazima.

Hata hivyo, alisema kuwa serikali itachukua hatua kwa makandarasi wa miradi ya maji watakaoshindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

# Wabunge wapaza sauti ukosefu dawa

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

WABUNGE wameishauri serikali kushughulikia suala la ukosefu wa dawa katika ngazi zote za afya kwa kuwa umekuwa kikwazo kupata huduma za uhakika.

Pia wameitaka serikali kuongeza watumishi wa afya pamoja na kuwapa motisha katika ngazi zote na kuanza utaratibu wa kutosubiri miundombinu ili kupeleka huduma za afya vijijini.

Wakichangia jana mjadala wa makadirio na mapato ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, walisema licha ya kuwapo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (CHF), lakini bado upatikanaji wa dawa ni kitendawili kikubwa. Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendegu, alisema ni kawaida wananchi kupata huduma halafu mwisho anaelekezwa dirisha la kununua dawa.

Alisema wakati mwingine kwenye zahanati, kituo au hospitali hakuna dawa na mgonjwa kulazimika kwenda umbali mrefu kwenye maduka yanayouza dawa kwa bima.

"Huu ni usumbufu mkubwa, lazima serikali iangalie namna ya kuboresha huduma hizi ili CHF na NHIF iwe kimbilio kwa wote, kama mtu atatumia gharama nyingi kufuata dawa hata mpango wa afya kwa wote hautafanikiwa sana ni muhimu dawa zikapatikana katika ngazi zote," alisema.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Christina Mzava, alisema zipo hospitali jijini Dar es Salaam hazitaki kuhudumia wajawazito wenye bima za afya wanaokwenda kutibiwa magonjwa mengine jambo ambalo siyo sawa na kuitaka serikali kuingilia kati.

"Ni muhimu serikali ikafuatilia suala hili, kama mama mjamzito anakosa huduma kwasababu ya hali yake kwa kuwa anatumia bima hii siyo sahihi na haikubaliki," alisema.

Mbunge wa Jimbo la Ukerewe (CCM), Joseph Mkundi, alisema ukosefu wa dawa na watumishi ni tatizo kubwa kiasi cha kusababisha wananchi wengi kukosa huduma za afya za uhakika.

Alito mfano wa jimbo lake kuwa hospitali ya wilaya inahudumia wagonjwa kutoka maeneo mengi ikiwamo Bunda, lakini bado huduma za afya siyo za kuridhisha na hakuna dawa kama inavyotakiwa.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Kisesa, Luaga Mpina, alisema licha ya jitihada za serikali kujenga zahanati, lakini kuna vijiji 6,527 havina huduma hiyo na kusababisha upatikanaji wa huduma za afya kuwa asilimia 50.3. Alitaka kufanyika mabadiliko ya kuwa na madaktari, wahudumu, vifaa tiba na dawa kwa huduma kutolewa kwenye majengo yanatofaa ya kijiji husika wakati miundombinu inasubiriwa, kwa kuwa kukosekana kwa miundombinu kunachelewesha huduma za afya kwa wananchi.

Pia alitaka serikali kuchukua hatua na kuwafikisha kwenye vyombo vya dola wanaothibitika kuiba dawa, kwa kuwa wanawanyima wananchi haki ya msingi.

## HABARI KITAIFA

# Rais Samia mgeni rasmi Baraza la Eid

**Na Maulid Mmbaga**



SHEKHE Mkuu wa Tanzania, Aboubakar Zuber, amesema Rais Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika Baraza la Eid ambalo kitaifa litafanyika mkoani Dar es Salaam.

Shekhe Mkuu aliyasema hayo jana Upanga, jijini Dar es Salaam katika hafla ya Iftari iliyoandaliwa na Mkuu wa Mkoa huo, Aboubakar Kunenge, kwa kuwafuturisha makundi maalumu ikiwamo watu wenye ulemavu, wajane na watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Pia Shekhe Zuber aliwataka waumini wa dini ya Kiislamu na wasio Waislamu kujitokeza kwa wingi kuhudhuria katika Baraza la Eid ambalo kwa mwaka huu litahutubiwa na Rais Samia ili kupata nafasi ya kusikiliza hotuba zitakazotolewa na mkuu huyo na viongozi wa kidini.

"Nimemwomba Rais Samia ahudhurie katika Baraza la Eid na amekubali kuwa mgeni wetu rasmi kwa hiyo ni vizuri Waislamu na wasiokuwa Waislamu tuhudhurie tuweze kusikia hotuba mbalimbali pamoja na yale ambayo Rais atatuelekeza katika siku hiyo," alisema. Pia alimshukuru mkuu wa mkoa huo kwa kuyafuturisha makundi yenye uhitaji na kuwakumbusha Watanzania wengine kuhusu suala la kuwatazama yatima pamoja na watu wengine wasiojiweza.

"Kwanza nashukuru na kumpongeza mkuu wa mkoa kwa kazi aliyoifanya kwa kuwakusanya watu wa aina mbalimbali wakiwamo yatima, wanawake wajane na maskini, pia kutualika na sisi viongozi wa dini, nimpongeze kwa kuwa amefanya jambo la kheri," alisema.

Aidha, kuna makundi katika jamii ambayo yamesahaulika na kuonekana kama si sehemu ya jamii au ni jamii duni ikiwamo yatima na wanawake wajane na watu wawe na utaratibu wa kuwakumbuka kwa kuwa wana mchango mkubwa katika jamii.




# DPP Biswalo ateuliwa kuwa jaji

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amefanya uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu na kumwongezea muda Jaji wa Mahakama ya Rufani, Patricia Saleh Fikirini, akiwamo Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Biswalo Mganga.

Katika taarifa iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam na kusainiwa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, ilisema kuwa Rais Samia, amewateua majaji saba wa Mahakama ya Rufani na Majaji 21 wa Mahakama Kuu.

Msigwa aliwataja Majaji wa Mahakama ya Rufani walioteuliwa ni kuwa ni Patricia Fikirini ambaye kabla ya uteuzi huu alikuwa Jaji Mfawidhi - Divisheni ya Biashara, Mahakama Kuu ya Tanzania (Dar es Salaam)

Wengine ni Penterine Kente ambaye kabla ya uteuzi huu alikuwa Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania (Iringa), Dk. Paul Kihwelo, ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto mkoani Tanga.

Aliwataja wengine kuwa ni Lucia Kairo, ambaye kabla ya uteuzi huo alikuwa Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania (Bukoba) na Lilian Mashaka ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Jaji Mfawidhi - Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Mahakama Kuu ya Tanzania (Dar es Salaam).

Wengine ni Issa Maige ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Jaji Mfawidhi - Divisheni ya Ardhi, Mahakama Kuu ya Tanzania (Dar es Salaam) na Abraham Mwampashi ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Alisema uteuzi wa Jaji wa Mahakama ya Rufani, Fikirini ulianza Mei 5, mwaka huu na wa Majaji wa Mahakama ya Rufani ulianza jana.

Katika taarifa hiyo, Rais Samia amemwongeza muda wa miaka miwili, Sivangilwa Mwangesi kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, kuanzia Februari, 15 mwaka huu.

Msigwa aliwataja Majaji wa Mahakama Kuu walioteuliwa kuwa ni Katarina Revocati, ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe, Biswalo Mganga ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Wengine ni Zahra Maruma ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Msajili, Mahakama ya Rufani Tanzania na Mkuu wa Kitengo cha Maboresho ya Mahakama (JDU) katika Wizara ya Katiba na Sheria, Devotha Kamuzora ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Msajili wa Baraza la Rufani la Kodi (TRAT), Dar es Salaam, Chaba John ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Msajili Mfawidhi, Masjala Kuu ya Mahakama Kuu Dar es Salaam.

Aliwataja wengine kuwa ni Lilian Itemba ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Wakili wa Serikali Mwandamizi katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Awamu Mbagwa ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofisi ya Mashtaka Dodoma na Ayoub Mwenda ambaye kabla ya uteuzi huu alikuwa Mkurugenzi Msaidizi, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka.

Wengine ni Nyigulile Mwaseba ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania (Dar es Salaam), John Nkwabi ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu (Arusha) na Safina Simfukwe ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Ardhi.

Msigwa aliwataja wengine ni David Nguyale ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Frank Mahimbali ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Msajili Mfawidhi, Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza na James Karayemaha ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza.

Wengine ni Emmanuel Ngigwana ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Msajili Baraza la Kodi, Abdi Kagomba ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Meneja wa Huduma za Sheria wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) na Arafa Msafiri ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Msaidizi wa Katibu wa Baraza la Mawaziri, Katiba na Sheria, Ofisi ya Rais Ikulu.

Pia katika uteuzi huo wamo Dk. Ubena John ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Mhadhiri na Mkuu wa Kitivo cha Sheria, Chuo Kikuu Mzumbe, Dk. Eliamini Laltaika ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Tumaini, Dk. Theodora Mwenegoha ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mwanabaraka Mnyukwa ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Mhadhiri wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama.

Alisema uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu ulianza jana na tarehe ya kuapishwa kwao pamoja na Mahakama ya Rufani itatangazwa baadaye.

# Rais ateta na Mkurugenzi UNFPA, Waziri Uingereza

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS Samia Suluhu Hassan jana amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Idadi ya Watu la Umoja wa Mataifa (UNFPA), Dk. Natalia Kanem, Ikulu, jijini Dar es Salaam.

Rais Samia ameishukuru UNFPA kwa ushirikiano wake mzuri na Tanzania katika utekelezaji wa miradi mbalimbali na kuunga mkono juhudi za serikali katika kukabiliana na ujauzito kwa mabinti wadogo, vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua, kukabiliana na ukatili wa kijinsia na ukeketaji.

Alimhakikishia Dk. Natalia kuwa atakuwa balozi mzuri wa kuhakikisha juhudi za kuwanusuru wanawake wanaojifungua wasipoteze maisha na kupiga vita mimba za utotoni na ameiomba UNFPA kuendelea kushirikiana na Tanzania ikiwamo kufadhili miradi ambayo inatekelezwa hapa nchini.

Nae Dk. Natalia alisema Umoja wa Mataifa wana matumaini makubwa na uongozi wa Rais Samia na amemhakikishia kuwa UNFPA itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kutekeleza miradi na shughuli mbalimbali za shirika hilo.

Wakati huo huo, Rais Samia amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza anayeshughulikia masuala ya Afrika, James Philip Duddridge.

Rais Samia amezikaribisha kampuni za Uingereza kuwekeza nchini Tanzania katika maeneo mbalimbali yenye fursa na kufurahishwa na ujio wa Duddridge ambao utafungua milango zaidi.

Kwa upande wake Duddridge alisema ana imani kubwa na uongozi wa Rais Samia kuwa utaendeleza kazi nzuri iliyofanywa na mtangulizi wake Hayati Dk. John Magufuli na amemhakikishia kuwa Uingereza itaendelea kushirikiana na Tanzania na kampuni za Uingereza zitaongeza uwekezaji hapa nchini.

## Chanzo foleni malori bandarini chatajwa

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI wa Bandari ya Dar es Salaam, Elihuruma Lema, amesema kutumika kwa mfumo wa kidijitali katika bandari hiyo ni mojawapo ya chanzo cha foleni za kila mara kwa malori yanayofika kuchukua mizigo.

Amesema kwa kipindi cha wiki mbili zilizopita mfumo huo ulikuwa ukifanyiwa matengenezo na baadhi ya huduma kusimama na kusababisha hali hiyo.

Hivi karibuni, kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa madereva wakiituhumu bandari hiyo, kuwa na kasi ndogo ya kuhudumia malori yanayofika kupakia na kupakua mizigo na kuwalazimu kusubiri zaidi ya siku mbili.

Akitoa ufafanuzi wa tuhuma hizo wakati akizungumza na mojawapo ya kituo cha redio, Lema alisema: "Katika wiki moja, mbili zilizopita tulikuwa tuna changamoto ya mfumo kulikuwa aidha kunafanyika 'maintanance' (matengenezo) ya mifumo inayohudumia bandarini kama TICTS."

Aliongeza: "Tunapofanya maboresho ya kimfumo huwa tunasimamisha operesheni na tunawatangazia wadau wote, lakini ukirejea mfumo bado kunakuwa na foleni".

Alibainisha kuwa inapotokea marekebisho ya mfumo wa kidijitali, mara chache hutumika njia mbadala ili kupunguza tatizo la foleni.

"Tatizo la foleni si kwamba halipo kwa asilimia 100, lipo lakini si madereva kukaa kwenye foleni kusubiri siku tatu ingawa wakati wa matengenezo huwa tunasitisha huduma. Tunaogopa kutumia mfumo wa kawaida kwa sababu unaweza kupoteza mizigo ya watu muda wowote na tukachafua mwonekano wetu," alisema Lema.

Alisema umuhimu wa kutumia mfumo wa kidijitali ni kwamba unasimamia uondoshaji mizigo kwa uwazi na kuonekana kwenye mifumo yote.

"Tatizo lingine la foleni linasababishwa na barabara inayoelekea bandarini, hivi sasa tunazipanua barabara hizo na zitakuwa tano, malengo yetu ni kufikia makusanyo ya Sh. trilioni moja".

Kadhalika, alisema ili kupunguza foleni bandarini, zipo bandari kavu ambazo hutumika kuhifadhi mizigo na kuondoa msongamano wa uondoshaji mizigo.

"Bandari kavu zinasaidia, zipo 14. Kwa sasa tunahifadhi mizigo takribani tani milioni 17 lakini kumbuka bandari ni ileile, hivyo ukibakia na mizigo yote inafanya bandari kufurika. Ili bandari ipumue, zinaondolewa kontena kwenda bandari kavu ambako wateja watafuata mizigo huko huko, si bandarini tena," alisema Lema.

Mmoja wa madereva wa malori ya mizigo, Boniface John, alisema mgawanyo wa taasisi za serikali ambazo huthibitisha kupakua na uondoshaji wa mizigo, husababisha kuchukua siku nyingi kufuatilia vibali.



Mhadhiri Msaidizi wa Chuo Kikuu Ardhi (ARU), Jonas Gervas (kulia), akifafanua jambo kuhusu utafiti anaoufanya wa kuangalia athari za utumiaji wa majitaka yaliyochakatwa kwenye udongo, kwa watu waliotembelea shamba darasa linalotumika kufanyia utafiti chuoni hapo, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mwinyi: Niliupata urais kwa bahati

**Na Sanula Athanas**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amebainisha kuwa aliupata urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa bahati.

Alisema Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alipanga Waziri Mkuu wa zamani, Hayati Moringe Sokoine, kuwa mrithi wake kwenye kiti hicho.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anabainisha kuwa urais wa nchi aliupata katika mazingira ya bahati kwa kuwa hakuwa chaguo la kwanza la Mwalimu Nyerere.

"Ni wazi kuwa Mwalimu Nyerere alilitafakari suala la mrithi wake kwa miaka mingi sana. Kwamba mimi nilikuwa Rais wa pili baada ya Mwalimu Nyerere ni bahati tu.

"Mwanzoni kabisa ninadhani Mwalimu Nyerere alikusudia kuwa Alhaj Aboud Jumbe Mwinyi aje kuongoza Tanzania baada yake. Ninadhani pia kuwa Aboud Jumbe mwenyewe alijiandaa kwa lengo hilo.

"Sidhani kuwa katika historia yupo Rais wa Zanzibar ambaye alizuru pembe za Tanzania kama alivyofanya yeye. Na alijaribu kila safari aambatane na viongozi tofauti kutoka Zanzibar, lengo lake likiwa Wazanzibari waijue vema nchi yao ya Tanzania," Mwinyi anasema.

Hata hivyo, 'Mzee Rukhsa' anabainisha kuwa baadaye alipojitokeza Sokoine, akaonyesha uhodari wa uongozi akiwa Waziri Mkuu, na hasa baada ya kuwa na shaka kidogo kuhusu Aboud Jumbe, Mwalimu Nyerere alikusudia kwa Sokoine aje kuwa mrithi wake.

Anasimulia kuwa baada ya kifo cha Sokoine kwenye ajali ya gari mwaka 1982, chaguo la Mwalimu likahamia kwa Dk. Salim Ahmed Salim na ndiyo maana akamteua kuwa Waziri Mkuu, ikiwa ni maandalizi ya kuja kuwa Rais wa Tanzania.

"Dk. Salim alipingwa na Wazanzibari wenziwe kwa hoja ya 'Hizbu'. Mpaka leo ninajiuliza ni lini Wazanzibari watajivua koti la historia linalowafanya watu waendelee kugawanyika kwa misingi ya kwamba familia hii walikuwa ASP na wengine walikuwa Hizbu na kadhalika," anasema.

Mwinyi anaendelea: "Sina uhakika Mwalimu Nyerere aliuonaje uongozi wangu wa Zanzibar, lakini ninapoangalia nyuma ninashawishika kuamini kwamba aliuona upole wangu kama upungufu wa uongozi.

"Lakini ndivyo Mwenyezi Mungu alivyoniumba; na kama ingeninyima nafasi ya kuwa Rais wa Tanzania hilo halikuwa jambo ambalo lingenisumbua sana. Ukweli ni kuwa niliridhika na urais wa Zanzibar, ambao nao sikuwa nimeutarajia kuutafuta."

Katika kitabu chake hicho, Mwinyi anasisitiza kuwa Watanzania wana bahati kubwa kwa kuwa na kiongozi mwenye maono, Hayati Mwalimu Nyerere.

"Mimi ni mzee sasa. Ninayaandika mambo haya ili vijana wa Kitanzania na wananchi kwa ujumla, waelewe tulikuwa na bahati kiasi gani kuwa na mtu wa sifa za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kama Rais mwanzilishi wa taifa letu huru.

"Alikuwa mfano wa kiongozi bora, mwenye kuona mbali na aliyejaliwa uelewa wa mambo mengi na mwenye hekima kubwa sana.

"Ni vyema kila mtu ajipime kwa vigezo hivi kabla hajatafuta uongozi wa taifa letu, na kuvizingatia awapo madarakani.

"Mtaelewa kwa nini baada ya kujikuta mimi ndiye wa kurithi Mwalimu Nyerere nilijihisi nimeelemewa na kujiona kama kichuguu nikijilinganisha naye niliyemwona kama Mlima Kilimanjaro," anasifu.

# DPP akosolewa kukusanya fedha za uhujumu uchumi

**Na Mary Geofrey**

WAKILI wa kujitegemea, Peter Madeleka, amesema Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) hapaswi kukusanya fedha za makosa ya uhujumu uchumi kwa mujibu wa kanuni ya 21, kanuni ndogo 3 (a) ya Kanuni ya Sheria za Kukiri Makosa (Pre Beginning) ya mwaka 2021.

Amesema kanuni hiyo imeeleza wazi kuwa, anayepaswa kukusanya fedha hizo ni Msajili wa Hazina na kwamba kwa kufanya hivyo anakiuka sheria.

Aliyaeleza hayo jana Dar es Salaam, katika mkutano wake na waandishi wa habari kuhusu makosa yanayofanywa kwenye Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi nchini, akiwa mmoja wa watuhumiwa waliokaa gerezani zaidi ya mwaka mmoja akakiri kosa, akalipa fidia na kuachiwa.

"DPP hajui kama hapaswi kupokea fedha kwa niaba ya hazina," alsema Wakili Madeleka.

Alisema Kanuni ya Sheria ya Kukiri Makosa (Pre Beginning) siyo inamtaka mtuhumiwa kulipa fedha kwa DPP bali inamtaka mtuhumiwa kufanya naye maridhiano ya kuomba kupunguziwa adhabu endapo atawataja watuhumiwa wenzake ili nao wakamatwe walipe fidia.

"DPP anaifanya 'Pre beginning' kama ni makubaliano ya kukusanya fedha wakati DPP siyo TRA (Mamlaka ya Mapato nchini)," alifafanua.

Kuhusu Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, alisema haina upungufu isipokuwa watendaji wanaoisimamia hawana uelewa wa kutosha katika kiisimamia na kuitekeleza.

"Ukiniuliza Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi mimi natakuambia ipo sawa kabisa tatizo lipo kwa vyombo vinavyoisimamia havina uelewa wa kutosha," alisema Wakili Madeleka.

Alisema Jeshi la Polisi ambao ndio wanaotakiwa kufanya upelelezi wa kesi hawana uelewa wa sheria hiyo ndio sababu wahusika wanasota magereza wakisubiria kukamilika.

Alishauri kuwa wanazosimamia sheria wanapaswa kuzisoma na kuzielewa kwanza kabla ya kuzitekeleza.

TANGAZO

NMB
Karibu yako

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 21 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ILIYOREKEBISHWA

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka wa wanahisa wa NMB utafanyika kwa njia ya mtandao saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa, Juni 4, 2021. Kampuni imerekebisha maazimio kwenye Taarifa ya Mkutano Mkuu na imeongeza ajenda nyingine. Kwahiyo Ajenda itakuwa kama ifuatavyo:**

21.1 MATANGAZO NA AKIDI

21.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO

21.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 20 ULIOFANYIKA TAREHE 5 JUNI 2020

21.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 20 WA WANAHISA

21.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020

21.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020

21.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI

21.8 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA MABADILIKO KWENYE KANUNI ZA KAMPUNI

21.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA KUJIUDHURU NA KUTEULIWA KWA WAKURUGENZI WA BODI

21.10 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DESEMBA 2021

21.11 MENGINEYO

**MAELEZO MUHIMU**

1. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria Mkutano lazima atume kwa njia ya mtandao nakala yake ya risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au kitambulisho chake au kadi yake ya benki.

2. Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni kama zilivyorekebishwa. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni (kwa njia ya mkono au mtandao) kabla ya saa 4 asubuhi Alhamisi ya tarehe 3 Juni 2021.

3. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria kikao atahudhuria kwa njia ya mtandao. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya NMB (www.nmbbank.co.tz).

4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 137 kwa kila hisa, inayoleta jumla ya shilingi 68.5 bilioni kutokana na faida ya mwaka 2020.

| **Tarehe za kuzingatia:** | |
|---|---|
| **Tarehe ya tangazo:** | **14 Mei 2021** |
| **Hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **14 Mei 2021** |
| **Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **2 Juni 2021** |
| **Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:** | **3 Juni 2021 nakuendelea** |
| **Daftari la wanahisa kufungwa:** | **7 Juni 2021** |
| **Malipo ya gawio kwa wanahisa:** | **kuanzia tarehe 16 Juni 2021** |

Kwa amri ya Bodi ya Wakurugenzi,

Lilian R. Komwihangiro
Katibu wa Kampuni
7 Mei 2021

www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uhaba wa maji saratani inayohitaji tiba ya kudumu

KATIKA michango ya wabunge kwenye makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji, walipaza sauti kuhusu ukosefu wa maji na upotevu mkubwa wa maji jambo linalosababisha wananchi wengi kukosa huduma hiyo.

Wapo wabunge waliosema kutokana na kukosekana kwa huduma hiyo kuna wananchi wanakunywa maji machafu ambayo hayastahili kunywewa na binadamu, lakini ni kutokana na ukosefu wa huduma hiyo.

Baadhi walikwenda mbali zaidi ya kushika Shilingi kwa madai kuwa upotevu wa maji unaongezeka kiasi cha kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 332, na kutaka hatua mahususi, ikiwamo kuunda kikosi kazi cha kufuatilia na kuja na suluhisho la kudumu.

Wabunge walisema hali ni mbaya zaidi vijijini kwa kuwa hakuna majisafi na salama na kwamba ule mpango wa kumtua ndoo mama bado haujafanikiwa kwa kuwa wanahangaika kutafuta maji.

Serikali inasema kwa sasa upatikanaji wa maji kwa mijini ni asilimia 80 na vijijini ni 73.2, lakini baadhi ya wabunge walionyesha wasiwasi wao kuhusu takwimu hizo kwa kuwa bado huduma ya maji ni changamoto kubwa.

Aidha, alisema fedha za miradi ya maji ni nyingi, lakini bado huduma hiyo haipatikani inavyotakiwa, huku hata maeneo ya mijini kukiwa na tatizo licha ya jitihada nyingi zilizofanyika.

Serikali imeahidi marekebisho makubwa kuhakikisha maji yanapatikana ikiwamo kusimamia kwa karibu miradi yote ya kutoa maji kwenye mito na ziwa kwa ajili ya kuyafikisha kwenye makazi ya watu.

Katika kukabiliana na uhaba huo serikali imeahidi kutekeleza miradi 1,527 ya maji katika maeneo ya vijijini na 114 maeneo ya mijini ikihusisha upanuzi na ukarabati wa miundombinu.

Pia serikali itachimba visima 516, kujenga mabwawa 33 hususani maeneo kame.

Ni hatua nzuri katika kujibu kilio cha wabunge, lakini bado inatakiwa kuwa na usimamizi wa karibu ili kuhakikisha miradi hiyo sio hewa bali yenye tija kubwa ya kuleta mabadiliko makubwa kwa wananchi.

Ni muhimu thamani ya fedha ikaonekana na kudhibiti mianya yote ya ubadhirifu ambayo ndiyo mchwa anayetafuna sekta ya maji nchini.

Kilio cha maji kimekuwa kikubwa na lengo la kumwezesha mwananchi kupata maji umbali usiozidi mita 400 inashindikana na sababu kubwa ni miradi mingi kutotoa maji kama inavyotakiwa.

Na katika kuonyesha kuwa kilio ni kikubwa Rais Samia Suluhu Hassan, alimtaka Waziri wa Maji kuongeza kasi ya usimamizi na huku akitumia usemi wa kiongozi huyo 'Ukinizingua nakuzingua' na kwamba ni vyema akawajibika mapema kabla hatua hazijachukuliwa.


Kwa msingi huo ni muhimu kuhakikisha huduma za maji zinapatikana ipasavyo, nia ya kumtua mama maji ionekane, kwani inashangaza hadi sasa upatikanaji wa maji hata kwa miji na majiji yenye vyanzo kuna changamoto kubwa ya huduma hiyo.

Hakuna ubishi kuwa maji yanahusiana moja kwa moja na suala la afya na iwapo maji yatapatikana kwa wakati maana yake maambukizi ya mgonjwa mengi yatadhibitiwa.

Lakini pamoja na jitihada hizo ni muhimu sana kasi ya kuelimisha wananchi ikaongezeka kwa kutumia maji kwa usahihi ili kuwezesha watumiaji wengine kupata huduma hiyo kwa uhakika zaidi.

Wapo wananchi bila uelewa wanatumia maji ya bomba ambayo yanaandaliwa kwa gharama kubwa kumwagilia bustani za maua, mboga na wengine kufyatulia matofali, wafuatiliwe na kuelimishwa umuhimu wa kuvuna maji ya mvua kwa kazi hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






Na Christina Mwakangale

## Muungwana Lazima Nilonge

# 'Asante Mzee Mwinyi unavyokuza Kiswahili'

UANDISHI wa vitabu kwa Kiswahili ni kati ya mikakati inayoweza kutumiwa na Tanzania kukuza lugha hiyo kwa vile ni njia mojawapo inayokiwezesha kusomwa na kizungumzwa na watu wengi zaidi duniani.

Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, ni mmoja wa viongozi ambao wameendelea kukikuza Kiswahili na safari hii ameandika kitabu chake kwa Kiswahili.

Mwinyi anayeweza kuitwa Baba wa Kiswahili ujuzi wake wa kuidumisha lugha hiyo unaonekana kila anapohutubia au kuzungumza na ameendelea kuwavutia wengi kutokana na umahiri wake wa kuongea na kutamka.

Mvuto wa hotuba zake hutokana na namna anavyoyatamka maneno kiufasaha na lafudhi yake ya Kiunguja huvutia zaidi.

Mwishoni mwa wiki kwenye uzinduzi kwa kitabu chake, kiitwacho 'Mzee Ruhksa: Safari ya Maisha Yangu', anaelezea masuala mbalimbali kwenye kitabu hicho kilichoandikwa kwa ufasaha kwa Kiswahili.

Uamuzi wa kuandika kitabu hicho kwa Kiswahili unalenga kufikia wasomaji wengi ambao wanaikubali kuwa ndiyo lugha yao ya mawasiliano.

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), linakikubali Kiswahili likisema kinazungumzwa na watu milioni 180 duniani.

Mzee Mwinyi akielezea baadhi ya sababu za Kiswahili kutumia kwenye kitabu chake anasema ni pamoja na kukikuza na kuunga mkono juhudi za serikali kukiendeleza.

Anasema Kiswahili amekitumia kwa sababu ya ujuzi alionao kwenye lugha hiyo na kwamba mwaka 1968, aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Baraza la Kiswahili na kuongeza: "Ujuzi wangu wa kutumia lugha hii umenifanya nichague Kiswahili kwenye kitabu changu."

Aidha, uzinduzi huo uliokwenda sambamba na kusherehekea miaka 96 ya kuzaliwa kwake uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan na katika kumshukuru anasema:

"Natambua uzito wa majukumu yako, lakini umekuja kunizindulia kitabu. Muda wa Rais kutokana na majukumu huwa ni mchache. Rais hana nafasi ya anasa, wakati wa marais ni mdogo," anasema Mzee Mwinyi, akitoa hotuba yake.

"Uliona kitabu hiki kina umuhimu wa kuzinduliwa kwenye awamu yako, kuwa Rais ni hidaya (kitu unachopewa bure). Nimetunukiwa uongozi bila rushwa wala uchawi ni mapenzi ya Mungu. Neema hizi ninazo kwa sababu ya hofu kwa Mwenyezi Mungu."

**"Natambua uzito wa majukumu yako, lakini umekuja kunizindulia kitabu. Muda wa Rais kutokana na majukumu huwa ni mchache. Rais hana nafasi ya anasa, wakati wa marais ni mdogo," anasema Mzee Mwinyi, akitoa hotuba yake.**

Aidha, Prof. Rwekaza Mukandala, akitoa muhtasari wa kitabu hicho, anasema, kati ya yale yaliyomo kwenye kitabu hicho ni historia ya tangu kuzaliwa, elimu, kazi hadi maisha ya kustaafu ya Mzee Rukhsa.

Anasema Mzee Mwinyi ambaye alizaliwa Mei 8, mwaka 1925, Kijiji Kivule, wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, kitabu chake kina maneno yapatayo 100,000 kilicho na maelezo ya ufasaha ya Kiswahili na kwamba lengo ni kufikia wasomaji wengi wa lugha hii.

Anasema Kiswahili kinachotambulika kwa baadhi ya nchi duniani, hususan Afrika, kimewaunganisha Watanzania tangu uhuru, kinatumika kwenye baadhi ya mikutano ya kimataifa barani Afrika ikiwamo mikutano ya Umoja wa Afrika (AU).

Mwaka 1986, Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO)lilipitisha azimio la kutumia Kiswahili kwenye vikao vyake vyote pia katika vile vya AU lugha hiyo inatambulika.

Inaelezwa na UNESCO kuwa Kiswahili kinazungumzwa hasa katika eneo la ukanda wa Afrika Mashariki, Kusini na Kati na mataifa ya Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Afrika ya Kati, Zambia, Comoro, Malawi, Afrika Kusini na Zimbabwe.

Lugha hii pia imeendelea kusambaa zaidi duniani kupitia vyombo vya habari hususan idhaa za kimataifa ikiwamo Sauti za Amerika (VOA), Ujerumani (DW), redio na televisheni ya BBC na Shirika la Redio na Televisheni la Uturuki (TRT).

Kukua kwa Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kunaelezwa kuwa ni fursa nyingine ya kukuza lugha hiyo kupitia majukwaa ya mitandaoni.

# Waonywa kuwaficha watoto wenye ulemavu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZAZI na walezi mkoani Shinyanga, wameonywa tabia ya kuwaficha ndani watoto wenye ulemavu na kutakiwa kuwapa haki kama wengine kwa kuwapeleka shule.

Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi binafsi ya watoto wenye ulemavu ya Brothers iliyopo Kitangili, Manispaa ya Shinyanga, Fransisco Bega, alisema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe alipotembelea shuleni hapo.

Alisema shule hiyo inafundisha watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali wakiwamo wenye mtindio wa ubongo, usonji na viungo na wamekuwa wakiwaibua kutoka kufichwa majumbani, pamoja na mitaani wakidhurura, kitendo ambacho ni ukatili na kumnyima mtoto haki zake ikiwamo elimu.

"Natoa tahadhari kwa wazazi ambao wanaficha watoto wao wenye ulemavu, wakiendelea kufanya hivyo mtoto huyo atakuwa dhaifu kabisa na hataweza kujitegemea maisha yake yote, lakini wakiwapeleka kwenye shule maalumu watabadilika na kuacha kuwategemezi sababu watakuwa na akili sawa na watoto wengine," alisema Bega.

"Mfano hawa watoto unaowaona hapa, walikuja hawajiwezi kwa chochote kabisa ikiwamo na kujisaidia ndani ya nguo, lakini baada ya kuanza kupata elimu, sasa hivi baadhi yao wanajua kusoma na kuandika na wameanza kujitegemea kwa kila kitu pamoja na kufua nguo zao wenyewe," aliongeza. Naye Ofisa elimu Shule za Msingi Manispaa ya Shinyanga, Neema Mkanga, aliwasisitiza wazazi kuwapeleka shule maalumu watoto wao wenye ulemavu, ikiwa walimu wapo wenye taaluma ya kuwafundisha na kutimiza ndoto zao.

Nao baadhi ya wazazi ambao wanasomesha watoto wao wenye ulemavu akiwamo Victoria Laurent, alisema baada ya kuanza kumpeleka mtoto wake shule, amebadilika kitabia na kimatendo, ambapo anajitegemea mwenyewe tofauti na hapo awali kipindi alipokuwa akikaa nyumbani.




Meneja Vifaa vya Intaneti wa Tigo, Mkumbo Myonga, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa simu mpya ya Infinix Hot 10t. Kulia ni Ofisa Uhusiano wa Infinix, Aisha Karupa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NIT, Chuo cha Ufundi Ethiopia kushirikiana

**Na Beatrice Moses**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimesaini mkataba wa makubaliano na Chuo cha Dire Dawa Polytechnic cha nchini Ethiopia katika mashirikiano yatakayolenga kushirikiana katika mafunzo ya ufundi na programu ya kubadilishana wakufunzi na wanafunzi na shughuli za utafiti.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa NIT Mhandisi Prof. Zacharia Mganilwa, alisema makubaliano kati ya vyuo hivi ni moja ya matokeo ya mradi wa EASTRIP, ambapo malengo makubwa ni kuleta mapinduzi kwenye elimu ya ufundi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Tumesaini makubaliano na Chuo cha Dire Dawa Polytechnic, ambapo kwa hivi sasa tutaweza kuanza kubadilishana walimu na wanafunzi," alisema.

Aliongeza: "Malengo makuu ya mradi huu ni kuvijengea vyuo hivyo vya ufundi uwezo ili viweze kutoa mafunzo bora na kuwapata wanafunzi wenye sifa stahiki ambazo zitawawezesha katika soko la ajira kwa kujiajiri ama kuajiriwa, pia fedha hizo za mradi zitatumika katika kujenga miundombinu ikiwamo madarasa, mabweni, karakana, ofisi za wahadhiri pamoja na watumishi wengine."

Mradi huo wa miaka mitano unafadhiliwa na Benki ya Dunia na kutekelezwa Tanzania, Ethiopia na Kenya, utaongeza hamasa kwa wanafunzi kujiunga na vyuo vya ufundi na kuboresha vyuo hivyo vya TVET.

Prof. Mganilwa alisema: "Mkataba huo wa umeainisha mambo ya ushirikiano kama kubadilishana walimu na wanafunzi pamoja na kusaidiana kujenga uwezo wa wanataaluma wa vyuo viwili hivi kwenye maeneo ambayo chuo kimoja kina uwezo zaidi, kuandaa mitaala ya pamoja na kufanya tafiti za pamoja."

Mkuu wa Chuo alisema kuwa katika mwaka huu wa masomo, NIT inatarajia kupokea wakufunzi wanne kutoka Chuo cha Dire Dawa Polytechnic.

Kwa mujibu wa Prof. Mhandisi Mganilwa, mwezi uliopita wataalamu wa TVET kutoka Ethiopia, Kenya na Tanzania walikutana Naivasha, Kenya, kujadili miongozo ya ubadilishanaji wa wanafunzi na wakufunzi.

Benki ya Dunia imetoa mkopo wa Sh. bilioni 175 kwa Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kuleta mapinduzi katika vyuo vinne vinavyotoa elimu ya ufundi hapa nchini.

## Tigo, Infinix wazindua simu ya kisasa zaidi

**Na Mwaqndishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo ikishirikiana na kampuni ya simu ya Infinix wamezindua simu mpya aina ya Infinix Hot 10t, ambayo ni kisasa zaidi kutoka kampuni ya Infinix.

Imeelezwa kuwa simu ya Infinix Hot 10t ina memori yenye ukubwa wa Gb 4 na Gb 68.

Meneja wa bidhaa za intaneti wa Tigo, Mkumbo Muyonga, alisema: "Katika mkakati wetu wa kuchochea matumizi ya simu janja na mtandao wa 4G nchini, tunaendelea kuungana na Infinix Tanzania ili kuhakikisha wateja wetu na Watanzania wote wanapata simu zenye uwezo wa 4G".

Katika uzinduzi huo jijiji Dar es Salaam jana, alisema: "Leo tumezindua simu ya kisasa zaidi 'Infinix Hot 10t' kwenye soko letu la Tanzania na sasa wateja wetu kote nchini wataweza kupata mtandao wa 4G kwa kupitia simu hizi."

Myonga aliongeza kuwa uzinduzi wa simu ya Infinix Hot 10t kwenye soko la Tanzania utaongeza thamani ya biashara na pia kuboresha maisha ya Watanzania wengi.

"Kwa kuongeza na kuhakikisha wateja wanapata huduma bora zaidi kwa gharama nafuu, simu hii ya Infinix Hot 10t itasaidia katika kuongeza idadi ya watumiaji wa simu janja nchini."

Kwa mujibu wa Myonga, simu hii itapatikana katika maduka yote ya Tigo nchini na inakuja ikiwa na kifurushi cha GB 78 kwa mwaka mzima bure.

Ofisa Uhusiano wa Infinix, Aisha Karupa, alisema: "Simu ya Infinix Hot 10t inakuja na kadi maalumu ya Helio G70 inayoiwezesha simu kuwa na uwezo mkubwa kwenye games, betri yenye uwezo wa 5000Ah inayoweza kukaa saa 24 ukiwa umewasha data."

**Meneja wa bidhaa za intaneti wa Tigo, Mkumbo Muyonga, alisema: "Katika mkakati wetu wa kuchochea matumizi ya simu janja na mtandao wa 4G nchini, tunaendelea kuungana na Infinix Tanzania ili kuhakikisha wateja wetu na Watanzania wote wanapata simu zenye uwezo wa 4G".**



Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, Nurdin Babu (katikati), akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi wa kisima cha maji chenye thamani ya Sh. milioni 220, kilichochimbwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) katika kijiji cha Machochwe, juzi, utakaonufaisha wakazi 12,000. Kushoto ni Mkurugenzi Mkazi wa Water Aid, Anna Mzinga na Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kutoa, kurudisha shilingi kulivyomchanganya mbunge

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Esther Bulaya, amejikuta hoja yake ya kutorudisha shilingi ikipotea baada ya kuchanganya kati ya kutoa na kurudisha.

Awali mbunge huyo alitoa shilingi kwenye kifungu cha mshahara wa Waziri wa Maji, hadi hoja ya upotevu wa maji itakaposhughulikiwa ipasavyo.

Hata hivyo, baada ya kuweka msimamo huo Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, kuwataka wabunge wanaotaka kuchangia, na licha ya michango hiyo aliendelea na msimamo wake hadi alipokosea na kusema harudishi shilingi badala ya kutoa na kutokana na makosa hayo hoja iliisha.

Wakichangia hoja hiyo, Mbunge wa Sikonge, Joseph Kakunda, alisema mikakati ya sera ya maji unazitaka mamlaka za maji mjini na RUWASA kufuatilia upotvu wa maji na wanaoiba maji na kujiunganishia wanachukuliwa hatua, na kwamba kwa kuwa kazi inafanyika ni kuongeza msisitizo.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Christine Ishengoma, alisema upotevu wa maji umepungua na jitihada zinaendelea na ameshachukua hatua.

Aidha, Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee, aliunga mkono hoja ya Bulaya na kufafanua kuwa mwaka 2010 asilimia 27 ya manunuzi ya nchi yalipelekwa sekta ya maji Sh. trilioni 2.7 zilienda chini (ardhini) bila kuwa na tija.

"Taarifa za CAG zinasema mamlaka hazipelekewi fedha zinadai shilingi bilioni 1.8, na zimeshindwa kwa miaka yote na fedha zinazidi kuongezeka, kuwe na kikosi kazi mahususi ili kusaidia taifa, haina maana kama tumewekeza mabilioni kwenye maji," alisema.

Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, alisema upotevu unaoruhusiwa ni asilimia 20, hali ya upotevu ilikuwa asilimia 44 na kutokana na juhudi imeshuka na sasa ni asilimia 36, na kwamba kuna jitihada kubwa inafanywa na wizara.

Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira na Muungano, Selemani Jafo, alisema ni muhimu kuangalia nia ya wizara ikaonekana katika kutatua tatizo hilo ikiwamo kubadili watendaji na kudhibiti wizi ikiwamo kushughulikiwa uchakavu huku kukiwa na mageuzi makubwa katika wizara hiyo.

"Tumetoa fedha Dar es Salaam kwa ajili ya kujenga mtandao wa maji wa kilomita 1,600," alisema.

# Wabunifu wajengewa mazingira

Na Renatha Msungu, DODOMA

TAASISI zinazohusika na uwekezaji zimetakiwa kutoa kipaumbele zaidi kwa wabunifu ambao bunifu zao zipo tayari sokoni ili kuwavutia wengi kuibuliwa na kutangaza kazi zao.

Mkurugenzi wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amosi Nungu, alibainisha hayo alipokuwa akifungua warsha iliyojumuisha wadau mbalimbali kutoka katika taaisisi za uwekezaji nchini.

Alisema miaka miwili mfululizo COSTECH imekuwa ikiweka mazingira wezeshi kwa wabunifu.

Alifafanua kuwa mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) utekelezaji wake unaangalia mambo matatu ambayo ni kuibua wabunifu, kuwatambua na kuwezesha wabunifu ikiwamo kuwaendeleza kupitia kazi zao.

Alisema jukumu la COSTECH ni kuhakikisha bunifu za wabunifu zinaibuliwa na kuboreshwa zaidi ili kutambulika kitaifa na kimataifa.

Naye Meneja Uhawilishaji wa COSTECH, Dk. Erasto Mlyuka, alisema sayansi, teknolojia na ubunifu ni nyenzo ambayo hutumika katika sekta rasmi na isio na kwamba serikali inatengeneza mazingira wezeshi kuhakikisha nyenzo hiyo inatumika kwa kufuata miongozo ya kisayansi.

Alisema kuna mwongozo wa kuwaibua wabunifu wanaotoka katika nyanja mbalimbali, Tume imepewa mamlaka ya kusimamia sayansi na teknolojia chini ya Wizara ya Elimu.

Mhandisi Bernad Lema alisema kazi kubwa ni kuwaibua wabunifu wadogo wanaochipukia lakini nguvu ipo kubwa katika masuala ya masoko.

Alisema mfumo wa masoko uliopo duniani ni mfumo shindano hivyo wabunifu wanatakiwa kupewa mbinu mbalimbali ambazo wataingia sokoni ili washindane na ili ubunifu uwe mzuri lazima uwekeze kwa nguvu.

Dk. Never Mwambela aliiomba serikali kuongeza fungu la kuwawezesha wabunifu kutokana na mahitaji kuwa katika shughuli za ubunifu wanazofanya.

"Tunaiomba serikali iongeze ufadhili na kutuunganisha wabunifu na masoko ili tusiendelee kubuni bali tuweze kuboresha maisha kupitia bunifu zetu," alisema Mwambela.

# Wawezeshwa kukamua mafuta ya alizeti

**Na Sabato Kasika**

KATIKA kuimarisha kilimo cha alizeti, kikundi cha kilimo cha Changamkeni cha Kijiji cha Masinono, Wilaya ya Musoma mkoani Mara, kimepewa mashine ya kukamua mafuta ya zao hilo yenye thamani ya Sh. milioni 35.

Mashine hiyo imekabidhiwa na Shirika la Maendeleo ya Kilimo na Ufugaji Musoma (SHIMAKIUMU), ambayo ina uwezo wa kukamua tani nne na nusu za alizeti kwa siku.

Ofisa Miradi wa shirika hilo, Elton Mtani, alisema SHIMAKIUMU inafanya kazi na vikundi 37 kwenye kata 11 za Bugwema, Bukima, Busambara, Bwasi, Murangi, Nyakatende, Musanja, Nyamrandirira, Etaro, Nyegina na Tegeruka.

"Kimsingi, tunatoa mashine kwa kuingia makubaliano ambayo yatanufaisha pande mbili kati ya shirika na vikundi vya wakulima ikiwa ni njia ya kuimarisha kilimo cha alizeti ambalo ni zao jipya huku," alisema Mtani.

Alifafanua kuwa mashine hizo zinahitaji mafuta na umeme, watu wa kuziendesha na walinzi, hivyo baada ya kutoa matumizi, faida inayopatikana ndiyo shirika lake na kikundi husika hugawana.

"Tunatoa mashine hizo ili kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha sekta ya kilimo, hasa kukuza na kustawisha kilimo cha zao hilo jipya ambalo linastawi kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Musoma," alisema. Katibu wa kikundi hicho cha Changamkeni, Gweina Matare, aliwaomba wadau wengine kukisaidia kikundi hicho kiweze kukamilisha ujenzi wa jengo kwa ajili ya kusimika mashine hiyo.

Alisema, wapo baadhi ya wadau wa kilimo akiwamo Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo ambaye amekisaidia kikundi hicho mbegu za mazao mbalimbali kama mtama, mahindi, mihogo na alizeti.

"Amefanya hivyo ili kuboresha kilimo jimboni mwake, hivyo nasi tunamshukuru kwa msaada huo unaolenga kuhakikisha wananchi wake wananufaika kwa kilimo cha mazao mbalimbali," alisema.

Mbunge Prof. Muhongo, alisema, ameshagawa majembe 85 ya kukokotwa na ng'ombe kwa vikundi mbalimbali ili kupanua mashamba ya wakulima ili kuinua kilimo jimboni mwake.

# Zimamoto yapokea taarifa 175 za moto shuleni miaka 4

BUNGE limeelezwa kuwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2016 hadi 2020, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilipokea taarifa 175 za matukio ya moto kwenye shule na 55 za masoko.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamza Khamis Chilo, aliyabainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Shally Raymond.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni matukio mangapi ya moto yametokea kwenye shule na masoko katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

"Je, uchunguzi ulifanyika ulibaini vyanzo vya moto huo ulisababishwa na nini?" Alihoji.

Akijibu, Naibu Waziri Chilo alisema katika uchunguzi mbalimbali za vyanzo vya matukio ya moto katika masoko na shuleni, jeshi hilo lilibaini vyanzo vya moto kuwa ni migogoro baina ya wanafunzi na menejimenti za shule.

Pia alisema matumizi ya umeme yasiyosahihi, uhalifu, uchomaji wa makusudi (hujuma), hitilafu za umeme, uchakavu wa mifumo ya umeme na uzembe kwa kuacha moto kwenye majiko ya mkaa.

"Ili kudhibiti matukio hayo, jeshi hilo linaendelea na mikakati ya kuzuia majanga ya moto kwa kufanya ukaguzi wa majengo na kutoa ushauri na mapendekezo ya kitaalamu yakiambatana na utoaji wa elimu ya kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto na pia kusisitiza kuwapo kwa vifaa vya awali vya kuzima moto na kung'amua moto na uwepo wa walinzi katika maeneo husika," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji serikali imejipangaje kuhakikisha jeshi hilo linafanya kazi kwa ufanisi.

"Je, serikali itatoa lini mafunzo ili wananchi wapate elimu ya kuzima moto?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha matukio ya moto yanapungua.

"Kutoa elimu kwa jamii tunaamini jamii ikipata taaluma majanga haya yatapungua, pia kukagua majengo ili kuelimisha namna ya kujikinga na majanga ya moto," alisema.

Hata hivyo, alisema mpango wao mwingine ni kuongeza visima ili yanapojitokeza majanga ya moto kuwepo na visima maalum vya kuchota maji ili kuokoa maisha ya watu.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (kushoto), akijadiliana jambo na Mbunge wa Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu Bungeni jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Nyumba 425 kuunganishiwa gesi Mtwara

SERIKALI imesema usambazaji wa gesi katika Mkoa wa Mtwara si wa kusuasua, na kwamba hadi kufikia Julai mwaka huu nyumba 425 zitakuwa zimeunganishwa na gesi majumbani.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Tunza Malapo.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua ni sababu zipi zinazosababisha kusuasua kwa usambazaji gesi kwa matumizi ya majumbani kwa wananchi wa Mtwara hususan Mtwara Mikindani.

"Sisi watu wa Mtwara kabla hatujapata gesi kwa matumizi yetu imepelekwa Dar es Salaam na watu wameunganishiwa majumbani, kwanini wameanza Dar es salaam badala ya Mtwara ambako gesi inatoka kwa kuwa na sisi tuna matumizi nayo," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema usambazaji wa gesi katika Mkoa wa Mtwara mwaka 2015 hadi sasa haujasuasua na kwamba mkoa huo na mikoa yote ya kusini inatumia umeme wa gesi pekee.

"Watumiaji wakubwa wa gesi nchini ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kiwanda cha saruji cha Dangote ambacho kipo Mtwara, ni moja ya faida inayopatikana kule, serikali imejitahidi kuhakikisha wananchi wa Mtwara wananufaika na gesi hii kwa sababu nishati ni kwa ajili ya Watanzania wote na itafika Dodoma," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji ni lini serikali itaunganisha mfumo wa gesi asilia kwa ajili ya kupata nishati ya kukaangia samaki katika Soko la Feri katika Manispaa ya Mtwara Mikindani.

Byabato akijibu swali hilo, alisema serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

inaendelea na kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika mikoa mbalimbali nchini ukiwamo Mkoa wa Mtwara kwa ajili ya matumizi ya viwandani, majumbani na taasisi za umma na binafsi.

"Katika Mkoa wa Mtwara mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa njia ya mabomba na vituo vya kuongeza mgandamizo wa gesi," alisema. Alieleza kuwa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika Soko la Feri katika Manispaa ya Mtwara Mikindani upo katika hatua ya kukamilisha usanifu wa kina wa kihandisi, utakaofuatiwa na hatua ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi huo. "Kazi ya usanifu inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2021 na ujenzi kuanza Desemba, 2021 na kukamilika Juni, 2022. Gharama za mradi ni takribani Sh. bilioni 10.11," alisema.




# Miundombinu hospitali rufani kukamilishwa kwa bil. 57/-

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, imetenga kiasi cha Sh. bilioni 57 kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu ya hospitali za rufani za mikoa ikiwamo Hospitali ya Katavi.

Naibu Waziri, Dk.Godwin Mollel, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mpanda Mjini (CCM), Sebastian Kapufi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa Hospitali ya Rufani Katavi kwani ujenzi huo unakwenda kwa kusuasua.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema kiasi cha Sh. bilioni 5.85 zitatumika kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Katavi ifikapo Januari 2022.

Aidha, alisema wizara inaendelea na ujenzi wa hospitali ya Mkoa wa Katavi ambapo kwa sasa ujenzi umekamilika kwa wastani wa asilimia 70.

Alifafanua ujenzi kwa upande wa maabara umefikia asilimia 98 na jengo kuu la hospitali umefikia asilimia 42.

Alisema mradi huo unagharimu Sh. bilioni 9.82 ambapo hadi sasa kiasi cha Sh. bilioni 3.97 kimetolewa na kutumika.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji serikali inawaeleza nini wananchi wa Katavi kuhusu ahadi zisizotekelezeka ikiwamo ahadi iliyotolewa na aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo, Ummy Mwalimu ya hospitali hiyo kuanza kutoa huduma Julai mwaka jana.

"Serikali inatoa kauli gani katika kuwanusuru wananchi wa Katavi kwa kukamilisha ujenzi huu kwa dharura kwa kuwa kuna hospitali zimejengwa kwa dharura kwa zaidi ya Sh. bilioni tisa?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema Sh. milioni 250 kwa mwaka zinatumika kwa ajili ya gari la wagonjwa kupeleka wagonjwa wa rufani kwenye hospitali za rufani.

Alikiri kuwa ahadi hiyo haijatekelezwa lakini Waziri wa Afya aliunda timu kuchunguza sababu za kuchelewesha ujenzi huo na atapewa mbunge.

"Lakini tumeandaa mpango mkakati kwamba ifikapo Januari mwaka 2022 hospitali hiyo itakamilika na kuondoa adha inayowakabili wananchi," alisema.

SAFARI YA MAISHA

Inavyoakisi kuibuka upya mageuzi kiuchumi, kisiasa

Ukurasa 12





Ukurasa 13

Ushirikiano na Kenya usiangalie kingine ila maslahi ya Tanzania



MELES ZENAWI:

Ukurasa 14

Muasi hadi Waziri Mkuu, aliacha shule kumwangusha Mengistu

siasa

JUMATANO MEI 12, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# Ahadi uteuzi usiojali itikadi

- Wadau wataka uanzishwe na katiba mpya
- Wahofia usilenge kuangamiza wapinzani

**Na Sabato Kasika**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameahidi ushirikishwaji wa wote katika kupanga safu za viongozi kujenga uchumi bila kujali itikadi, dini wala jinsia na kuahidi kuteua Mtanzania yeyote mwenye sifa za uongozi bora.

Anasema atakachozingatia katika uteuzi wake ni weledi, umahiri na uwezo wa kufanyakazi yenye manufaa kwa taifa, hayo yakijiri katika mkutano wake na wazee wa mkoa wa Dar es Salaam, uliofanyika wiki iliyopita na kuahidi kufanya mabadiliko hayo kwa lengo la kujenga na siyo kubomoa.

"Huko mbele wakati nikiendelea kusuka serikali, sitaangalia itikadi ya mtu nitakayeona ana uwezo wa kusaidia taifa lake katika eneo fulani, nitamteua afanye kazi bila kujali anatoka chama gani," Rais Samia anasema na kuongeza kuwa ili mradi mtu huyo hana dosari ya kiusalama wala ya kimadili anateuliwa.

Nipashe inazungumza na baadhi ya wadau na wachambuzi wa siasa kupata maoni yao kuhusu mtazamo wao akiwamo mjumbe wa Baraza Kuu la Chama cha Wananchi (CUF), Abdul Kambaya, anayesema dhamira ya Rais Samia ni njema lakini ni vyema kupata baraka za kisheria.

"Kwa hotuba ya Rais Samia kwa wazee wa Dar es Salaam, basi ili kuendeleza dhamira njema, kuna haja na kuanzisha mchakato wa katiba mpya kwa lengo la kuyahalalisha maono kisheria na kuleta ufanisi wa kauli yake," anasema.

"Kwa hakika hii si dhamira yenye lengo la kuimarisha uchumi tu bali pia kuleta umoja na upendo miongoni mwa Watanzania, lakini ni muhimu iwe na baraka za kisheria Rais aanzishe sasa mchakato wa kupata katiba mpya baada ya kukwama mwaka 2014 na masuala hayo yaainishwe kikatiba," anasema Kambaya.



Mjumbe wa Baraza Kuu la CUF, Abdul Kambaya. **PICHA: MTANDAO**

Kambaya anatolea mfano wa muafaka wa Zanzibar akisema Jakaya Kikwete, wakati huo akiongoza awamu ya nne alipohutubia Bunge mwaka 2005, alieleza kusikitishwa kwake na hali ya kisiasa Zanzibar na kuahidi kuumaliza mkwamo huo.

Anamnukuu Kikwete akisema kuwa Tanzania haiwezi kuendelea kuwa mtumwa wa historia inayoleta mgogoro usio wa lazima ndipo alipoanzisha mabadiliko ya katiba ya Zanzibar yaliyofanikisha kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) ambayo hata sasa inaendelea kushirikisha pande zote.

**KATIBA INARUHUSU**

Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia kilichoko Kurasini Dar es Salaam, Godwin Gonde, anasema kauli ya Rais ni jambo la kawaida si geni na kwamba inawezekana kwa maelezo kuwa katiba inaruhusu.

"Ibara ya 51 (2), inaweka wazi jinsi ambavyo inawezekana Rais kuteua yeyote kutoka chama chochote cha siasa bila kukiathiri katiba ya nchi. Ibara inasema; Mapema iwezekanavyo ndani ya siku 14, baada ya kushika madaraka yake, Rais atamteua mbunge wa kuchaguliwa kutoka katika jimbo la uchaguzi anayetokana na chama cha siasa chenye wabunge wengi zaidi bungeni au kama hakuna chama chenye wabunge wengi zaidi, atamteua anayeelekea kuungwa mkono na wabunge walio wengi kuwa Waziri Mkuu... naye hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na bunge kwa azimio litakaloungwa mkono na kura za wabunge walio wengi." Kwa mfano huo Rais anaweza kuteua mbunge yeyote.

Gonde anasema tangu Rais atangaze nia hiyo baadhi ya watu wamekuwa wakihoji na kudai, huenda akaua upinzani, kwa madai kwamba watakaoteuliwa watalazimika kuhama vyama vyao.

"Sioni tatizo, katiba iko wazi, labda atakayeteuliwa na kuhama, afanye hivyo kwa mapenzi yake kama ambavyo baadhi ya watu waliteuliwa na kuhama, lakini wanaweza kufanya kazi wakiwa katika vyama vyao," anasema.

Anasema, ibara inatoa mfano wa Waziri Mkuu, inawezekana hata kwa mtu mwingine kulingana na wingi wa wanachama au anayeelekea kuungwa mkono na wengine walio wengi.


Gonde anafafanua kuwa, kwa kutumia ibara hiyo, Rais anaweza kuteua mtu kutoka chama chochote na kufanya naye kazi bila kuhama kwa kwamba wanasiasa wasiwe na hofu za na hilo.

INAENDELEA UK.12

KITABU SAFARI YA MAISHA




Rais Samia Suluhu Hassan, akinyanyua juu kitabu cha Historia ya Maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi, baada ya kukizindua katika hafla iliyofanyika katika ukumbi wa Mwalimu Nyerere Convention Centre jijini Dar es Salaam Mei 8, 2021. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**




Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi, akinyanyua juu kitabu cha historia ya maisha yake baada ya kuzinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

# Inavyoakisi kuibuka upya mageuzi kiuchumi, kisiasa

**Na Ani Jozeni**

YAPO matukio yanayosaidia kuweka mkazo na kuinua mshikamano kuhusu dira na mwelekeo nchini, na majuzi uzinduzi wa kitabu cha maisha ya Ali Hassan Mwinyi, Rais wa awamu ya pili, ni miongoni mwa hayo.

Kitabu cha Mzee Rukhsa ni baraka ya kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan, kuweka mkazo katika ajenda ya mageuzi ya sera za uchumi, kuzidi 'kukandamiza' utukufu unaopaukа wa taasisi za dola katika kusimamia uchumi, sifa na nafasi ya juu kisera iliyodumu kwa miongo mitatu sasa.

Rais Samia ambaye mwishoni mwa wiki alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo, aliweka mkazo kwa picha iliyosahaulika ya Rais Mwinyi kuwa

**BABA WA MAGEUZI**

Sababu ya kusahaulika kwa nafasi hiyo ni kuwa siyo watawala serikalini au wasomi wa maeneo ya uchumi, mifumo ya jamii, siasa au uendeshaji biashara waliofurahia mageuzi ya uchumi wakati wa awamu ya pili.

> Miaka 28 baadaye suala hili liko mezani, jinsi ya kujenga uchumi kiufanisi, kwa msingi wa kulegeza masharti ya biashara...

Waliona kuwa ni kuzitii taasisi za fedha za kimataifa hasa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia (WB).

Utawala serikalini na utii kisiasa kwa Rais Mwinyi ulidumu kwa miaka saba, 1985 hadi 1992, halafu Mei 1993 ukatoka waraka, 'Rais Mwinyi aache sera yake ya kuuza nchi. Miaka 28 baadaye suala hili liko mezani, jinsi ya kujenga uchumi kiufanisi, kwa msingi wa kulegeza masharti ya biashara na kupunguza ukuu wa taasisi za dola.

Kabla ya uzinduzi wa kitabu cha Mwinyi, Rais aliwahutubia wazee wa Dar es Salaam na akisisitiza ulazima wa kufanya mabadiliko makubwa katika sera za uchumi na mfumo wa uongozi, akigusia nia ya kufanya uteuzi wa kiongozi kutoka kokote bila kujali anayeteuliwa ni wa chama gani.

Hayo yaliendana na Rais Mwinyi kuwa mwasisi wa mfumo wa vyama vingi, ingawa hata katika kitabu chenyewe, inaonyesha ni Mwalimu Nyerere alitetea zaidi mabadiliko, si yeye.

Katika hafla hiyo, Profesa Rwekaza Mukandala mtafiti wa masuala ya siasa na Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mstaafu anatoa mapitio au muhtasari wa kitabu hicho.

Ni kitabu cha pili kutayarishwa kwa kiongozi mkuu wa nchi aliyestaafu, kwa kushirikiana na Taasisi ya Uongozi, ambayo kwa muda mrefu sasa imeongozwa na Profesa Joseph Semboja, ambaye mwaka 2019 alisimamia kukamilika na kuzinduliwa kwa kitabu cha maisha ya mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa.

Katika hafla hiyo Rais Samia akaelezwa kuwa mstaafu Jakaya Kikwete yuko mbioni kukamilisha kitabu kuhusu maisha yake.

Rais Samia anasema kuwa kitabu cha maisha ya Mzee Rukhsa kilikuwa kizinduliwe na Rais John Magufuli, wakati wa uhai wake, hivyo jambo hilo ikabidi kuandaliwa upya.

Kitabu cha Mzee Rukhsa, kimezinduliwa katika mazingira muafaka zaidi wakati huu wa kushangilia uongozi wa Mzee Mwinyi kuliko awali, kwani eneo ambalo alifaulu zaidi ni kufanikisha mageuzi ya kina ya uchumi na kuingiza demokrasia ya vyama vingi.

Ni sawa na wakati huu ambao kuna mikakati halisi ya kurejesha mwelekeo huo. Awamu ya tano ya Magufuli iliendana na awamu ya kwanza ya Mwalimu Julius Nyerere, kwa maana ya msisitizo wa dola kusimamia uchumi na kurudisha bila kurasimisha mfumo wa chama kimoja.

Suala jingine lililofanya uzinduzi huu uendane na muktadha wa mhusika kwa maisha ya Mzee Ruksa ni kuwa kilizinduliwa kwenye 'birthday' yake, akifikisha miaka 96, jambo ambalo liliongeza shangwe na taadhima maalum katika hafla hiyo. Jambo jingine ambalo alitilia mkazo Rais Samia akimnukuu Mzee Mwinyi ni kuwa uongozi wa juu haupiganiwi.

Anasema ni baraka tu kutoka mbinguni. Kitabu kinatoa nukuu ya William Shakespeare, bingwa wa fasihi na tamthilia zilizodumu karne sita huko Uingereza, akisema uongozi uko aina tatu.

Upo wa kuzaliwa nao, wa kuhangaikia na wa kutwishwa. Mzee Rhuksa na Rais Samia kwa kiasi fulani, wanaainisha kuwepo kundi la tatu kwani hawakupigania uongozi wowote ule ila walipewa.

Wakati hayati Rais Mkapa alisifiwa katika uzinduzi wa kitabu cha maisha yake na hasa katika wasifu wa maisha yake alipofariki kuwa aliasisi na kusimamia kuundwa kwa taasisi muhimu za nchi na kuratibu sekta tofauti, bado haibadili kilichosema katika hafla ya juzi.

Tena labda itahitajika kwa wale watakaosoma kitabu cha maisha ya Ali Hassan Mwinyi ambao bila shaka watakuwa wengi zaidi kwani kimeandikwa kwa Kiswahili watafakari mahusiano ya kuwa baba wa mageuzi ya uchumi na kuwa mwasisi wa taasisi maridhawa za nchi.

Siyo watu wengi wanaweza kupima kwa kina nafasi ya taasisi hizi katika mageuzi ya uchumi na mkwamo wa maendeleo, hata kurudisha ajenda ya mageuzi sasa.

Ni wazi kuwa uongozi wa juu uliopo haukuomba jambo hili lifanyike sasa, kwa maana ya muda ambao kitabu hicho kimekamilika na mazingira yake ya kisiasa, lakini kumekuwa na kushabihiana.

# Ahadi uteuzi usiojali itikadi za kisiasa

**INATOKA UK.11**

**UMAKINI NI MUHIMU**

Maggid Mjengwa anasema, lengo la Rais ni zuri, kwa maelezo kwamba linalenga kukuza na kupanua demokrasia nchini, hivyo hatua kuteua wapinzani kutasaidia kama kutakuwapo utaratibu maalum.

"Lakini vilevile hatua hiyo inaweza kuwa kete nzuri kwa CCM ya kuua upinzani iwapo utaratibu utakuwa kama ule wa miaka ya nyuma wanachama wa upinzani kupewa vyao na kuhama vyama vyao," anaonya Mjengwa.

Anasema, ikiwezekana uwe ni utaratibu wa kikatiba ili mpinzani anapohitajika kuingizwa serikalini, viongozi wa chama husika washirikishwe ili kuepuka mtafaruku ndani ya vyama vya upinzani.

"Nikumbushe pia kwamba, kila chama kina itikadi yake na ni kama imani, ambayo mtu kuibadili ni vigumu, na kwa mwanachama aliyeiva inakuwa ni vigumu kusalati itikadi yake," anasema.

Mjengwa anasema, labda itikadi za vyama zifanane, ndipo vinaweza kuungana na kuunda serikali au kushirikiana katika kazi na kwamba vinginevyo, mipango ya Rais inaweza kuua upinzani.

"Kwa mfano Uingereza, ni vigumu mwanachama wa Conservatives kuhamia Labour kwa sababu itikadi hazifanani, hivyo hata kwa hili analosema, likifanikiwa, upinzani utakuwa mashakani," anaonya.

Anafafanua kuwa lengo la chama cha siasa ni kushika dola kwa njia halali ya uchaguzi, sasa linapokuja suala la wanachama wa vyama vya upinzani kuingizwa serikalini, maana yake ni kuviua.

UCHAMBUZI

# Ushirikiano na Kenya usiangalie kingine ila maslahi ya Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameitembelea Kenya katika ziara inayoelezwa kuwa imefungua ukurasa mpya wa mtangamano unaoashiria kuimarisha udugu na ujirani baina ya mataifa hayo.

Akiwa Nairobi anahutubia wafanyabiashara na wabunge wa bunge la kitaifa na la seneti wote akiwahakikishia kuwa anatamani kuona uhusiano endelevu kati ya Kenya na Tanzania.

Anawaambia wabunge: "Binafsi nashangazwa sana na wale wanaodhani Kenya na Tanzania ni wapinzani. Mbaya zaidi ni kule kuamini kwao kwamba hilo linawezekana tu mmoja wetu kumwangusha mwenzake. Hawa ni watu wenye mioyo ya choyo, maono mafupi na akili mbovu."

"Ni bahati mbaya kuwa wapo katika pande zote mbili, Kenya na Tanzania. Hutokea pia wachache wao wakawa ni watumishi wa serikali na hata wanasiasa wa pande mbili..."

Aidha, Rais anaahidi kuwa awamu ya sita itahakikisha kuwa Kenya inabaki kuwa ndugu, jirani na mshirika wa mkakati, ahadi ambayo baadhi ya wadau wanaisifu na kuona kuwa ni mwanzo wa kudumisha ushirikiano, lakini ni lazima ulenge kwenye maslahi ya Watanzania na zaidi ya hapo utakuwa hauna tija.

Akizungumza na Nipashe kuhusu hotuba na ziara ya Rais Nairobi, Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba Tanzania, (JUKATA) Bob Wangwe, anakumbusha haya:

"Jambo la muhimu pamoja na udugu na ujirani wetu na Kenya lolote lazima liwe ni maslahi ya Watanzania. Hiki ndicho kiwe kipaumbele katika kila uamuzi tunaochukua kama nchi."


Anaunga mkono ziara ya Rais Samia, akisema ni muhimu kwani itazisaidia nchi zote mbili kujenga uelewano ambao ni muhimu katika maendeleo ya mataifa hayo kwani Kenya na Tanzania zinategemeana.

Hata hivyo, anapoulizwa kuhusu hofu kuwa mara nyingi ushirikiano umekuwa na wasiwasi, anasema hofu hazikosekani ni lazima ziwepo kwani kila nchi inafikiria zaidi kutumia fursa inazopata kwa ajili ya kuendeleza mipango na mikakati yake, hivyo kipaumbele cha kuwanufaisha Watanzania ndicho kiwe suala la msingi.

Anakumbusha kuwa ili kuwa na uhusiano na ushirikiano wenye tija kwa pande zote mbili au 'win win situation' ni vyema serikali mbili zingine kwenye makubaliano kwa kutambua na kuzingatia tofauti baina zao.

Anapoulizwa kuhusu suala la baadhi ya Watanzania kuona kuwa kuna mambo yanayofanywa na majirani zao ambayo yanakwenda tofauti na mustakabali wa taifa lao, mfano kutangaza Mlima Kilimanjaro kuwa uko nchi jirani.

Aidha, mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa soko kuu la bidhaa za Tanzania



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa na mwenyeji wake Rais Uhuru Kenyatta, alipoitembelea Kenya hivi kabribuni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Mkurugenzi Mtendaji wa JUKATA, Bob Wangwe.

kinyume cha utaratibu Wangwe anasema.

"Inapotokea nchi inavunja makubaliano ya pamoja ya jumuiya hiyo ni jukumu kwa jumuiya kuwajibika katika kulinda misingi na makubaliano ya pamoja. Siyo vyema kutupiana lawama."

Mkurugenzi Mtendaji wa JUKATA, anahimiza kuendelea kukuza uelewano wenye tija baina ya nchi wanachama na hili ndilo litakaloleta utashi wa pamoja katika kuheshimu misingi wanachama waliojiwekea.

**KUTAZAMA TOFAUTI**

Wangwe akizungumzia ahadi za Kenya kwa Watanzania mfano Rais Uhuru Kenyatta, anaahidi kwamba nchi yake iko tayari kupokea Watanzania kuendesha shughuli zao bila vibali vya ukazi na kazi.

Anafafanua kuwa kwa Kenya ni sawa lakini Tanzania ikiruhusu hilo itakuwa imefanya kosa kubwa kwa kuwa bado watu wake hawajaandaliwa.

"Hii itakuwa sahihi kama tukifanya hivyo kwa wawekezaji hasa wa daraja "A". Tanzania tuna ardhi kubwa kweli, lakini ni kwa ajili ya Watanzania. Leo tukibadilisha mifumo yetu ya kisheria kwa lengo la "kuhonga" ardhi yetu kwa msamiati wa udugu na ujirani tutakuwa tumewakosea sana wajukuu zetu na wazee wetu ambao walitulindia ardhi hiyo."

Anaeleza kuwa ni muhimu kushirikiana lakini maslahi ya Watanzania yawe ndicho kipaumbele bila kujali kingine na mipango ifanyike kwa kuangalia tofauti zilizopo baina ya washirika.

Rais anaahidi kuboresha na kuondoa vikwazo vya biashara vilivyopo Tanzania vinavyoathiri ushirikiano kati ya wafanyabiashara wa mataifa hayo akiahidi kuvishughulikia na ili kuwepo na biashara isiyo na vikwazo, lengo liwe ushirikiano unaoleta tija.

Wangwe anazidi kukumbusha kuwa katika hatua yoyote lazima suala la tofauti ya nchi zote mbili lizingatiwe ili mataifa yote yanufaike.

"Ni bahati mbaya sana kwamba hatua zetu Watanzania kama

> "Jambo la muhimu pamoja na udugu na ujirani wetu na Kenya lolote lazima liwe ni maslahi ya Watanzania. Hiki ndicho kiwe kipaumbele katika kila uamuzi tunaochukua kama nchi.

nchi bado ni chache ukilinganisha na Kenya, hivyo lazima tushirikiane kwa kutambua hili."

**MAONI YA WADAU**

Mmoja wa wakulima wanaozungumzia biashara baina ya Kenya na Tanzania anaomba serikali itazame sheria za kununua mazao mabichi mashambani.

Wakulima Arnold Mkupete na Kulaga Ngomale, wanasema wanalima maeneo ya Mvuha na kijiji chao kinazungukwa na maji ya Mto Mvuha na mara nyingi wanafikiwa na wakulima kutoka nchi jirani ambao wananunua mazao mashambani tena kwa bei kiduchu.

Mkupete anasema: "Kuna maeneo ambayo yanawaumiza wakulima ni wageni wanaofika vijijini kununua mazao mabichi. Kwa mfano wananunua iliki mbichi kwa bei ndogo sana. Tunaomba hili likaangaliwe."

Anaungwa mkono na Kulaga anayeshauri kuwa kuwe na magulio vijijini kama yalivyo kwenye kuuza na kununua korosho, ufuta na pamba na serikali itoe bei elekezi ili wakulima wafaidike badala ya kuacha mambo yabaki kama yalivyo ambayo hayana tija.

Baadhi ya wakulima wengine wanaozungumzia biashara za mashambani ni wa kutoka Kilimanjaro na Arusha wanaosema wafanyabiashara majirani wananunua maparachichi, mbaazi, vitunguu na mazao mengi kwa bei ndogo na kutaka kuwe na utaratibu mpya wenye tija mbali na kutaka magulio.

Wanashauri kuwe na utaratibu wa kutaja asili ya bidhaa (place of origin) na serikali kusaidia wakulima na Watanzania kupata soko la bidhaa nje moja kwa moja badala ya kuachia wageni wanaozinunua na kuziuza ughaibuni kwa faida kubwa kama za wakati walizinunua vijijini kwa bei kiduchu.

JUKWAA LA UONGOZI

# MELES ZENAWI

- Muasi hadi Waziri Mkuu, aliacha shule kumwangusha Mengistu
- Alimmaliza kila aliyempinga, alivaa sura nyingi ubabe na utetezi

**Na Mwandishi Wetu**

MELES Zenawi Asres, alikuwa Waziri Mkuu wa Ethiopia kuanzia mwaka 1995 hadi kifo chake kilichotokea 2012.

Kabla ya kushika wadhifa huo kuanzia 1989, alikuwa kiongozi wa chama cha ukombozi cha Watigray (TPLF) na kiongozi wa chama cha EPDRF tangu kilipoundwa mwaka 1991.

Kuanzia mwaka 1995, alikuwa Rais wa Serikali ya Mpito mwaka 1991 hadi 1995. Zenawi alifariki dunia Agosti 20, 2012 mjini Brussels, Ubelgiji, alikokuwa amelazwa ukiwa ni mwendelezo wa viongozi wa Afrika kutibiwa nje ya nchi kutokana na kukosekana kwa hospitali za kisasa na wataalamu bora katika mataifa yao.

Waziri Mkuu huyo wa Ethiopia miezi michache kabla ya kifo chake, alipiga marufuku maandamano nchini humo kufuatia uchaguzi mkuu hatua aliyoichukua Mei mwaka 2012.

Akizungumza kupitia Televisheni ya Taifa Zenawi alisema vikosi vya usalama mjini Addis Ababa vitakuwa vikipokea amri kutoka kwake moja kwa moja wakati huo akitamba kuwa ndiye Amiri Jeshi Mkuu.

Katika uchaguzi huo idadi kubwa ya Waethiopia walijitokeza huku Zenawi na chama chake cha Ethiopian People's Revolutionary Democratic Front kikitangazwa mshindi kama kawaida.

Wakati hayo yakitokea upinzani ulitishia kuyapinga matokeo ya uchaguzi huo kwa madai ya udanganyifu na kutoa vitisho.



Aliyekuwa Waziri Mkuu wa Ethiopia, Meles Zenawi Asres. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### KUZALIWA

Zenawi alizaliwa Mei 8, 1955 na kama angekuwa anaishi angekuwa na miaka 66. Baba yake alikuwa mkulima mdogo aliyeishi huko Adua, kaskazini mwa Ethiopia. Baadaye alipewa jina la "Meles" likimuenzi mpigania uhuru mmoja.

Alihitimu kutoka shule ya watu wenye vipaji maalumu na kupata shahada mbili za uzamili, akisoma kwa njia ya posta. Elimu aliyoipata, ilimpa nafasi ya kutoa hotuba za kitaaluma mbele ya wageni wa serikali ya nchi yake.

Waziri Mkuu huyo alisomea udaktari, Meles, alianza kujihusisha na masuala ya kisiasa.

Alijiunga na makundi yanayofuata mafundisho ya mwanafalsafa Karl Marx na kushirikiana na vuguvugu lililosababisha kung'olewa madarakani kwa mfalme Haile Selassie mwaka 1974.

> "Hivi mnafahamu kwamba nchi yetu ilikuwa na utamaduni ulioendelea kabisa wakati ninyi mlikuwa bado wawindaji na watu wakukusanya matunda na mboga msituni?

### MUASI AWA WAZIRI MKUU

Baada ya kiongozi wa kijeshi wa nchi hiyo, Mengistu Haile Mariam kuingia madarakani, Meles alikatisha masomo yake na kuingia katika vita vya chini kwa chini dhidi ya Mengistu ili kumwangusha.



Waziri Mkuu wa Ethiopia aliyepinduliwa, Mengistu Haile Mariam.

Kwa zaidi ya miaka 10, kundi lake la waasi liitwalo Tigray's People Liberation Front (TPLF), lilifanya mashambulizi katika milima ya Tigray.

Ilipofika Mei 1991, waasi wa kundi la TPLF, wakisaidiwa na Marekani, waliuteka mji mkuu wa Addis Ababa.

Meles, aliyekuwa rais wa kipindi cha mpito, alipoulizwa na gazeti la Ujerumani la Frankfurter Rundschau kama nchi yake iko tayari kwa demokrasia alijibu:

"Hivi mnafahamu kwamba nchi yetu ilikuwa na utamaduni ulioendelea kabisa wakati ninyi mlikuwa bado wawindaji na watu wakukusanya matunda na mboga msituni?"

Kijana huyo alichaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa Ethiopia kupitia muungano wa vyama uliokuwa madarakani tangu mwaka 1991, Ethiopian Peoples' Revolutionary Democratic Front (EPRDF), kiongozi huyo aliongoza kazi ya kuwasaka washirika wa Mengistu.

Tangu kuingia madarakani kwa Meles, mashirika ya kutetea haki za binadamu yamekuwa yakilaani sera zake, hasa juu ya namna alivyoiendesha nchi yake katika miaka ya 1990 lilipotokea janga la njaa.

### ALAMA MBAYA

Anadaiwa kuwa tukio la kwanza baya ni vita kati ya Ethiopia na jirani yake Eritrea, vilivyotokea kati ya mwaka 1998 na 2000. Jingine ni madai ya wizi wa kura katika uchaguzi mkuu uliofanyika mwaka 2005.

Aidha, ilidaiwa watu wapatao 200 waliuawa kwenye maandamano ya kupinga matokeo ya uchaguzi huo. Wakati Meles alipokuwa akijisifu kuwapatia raia wake haki ya kufanya uchaguzi aliouita wa haki, maafisa wake wa usalama waliwashambulia kwa risasi wanafunzi waliokuwa wakiandamana na kuwaua.

Baada ya uchaguzi wa mwaka 2005, mashirika ya kutetea haki za binadamu yaliripoti juu ya rushwa na matumizi ya nguvu dhidi ya wapinzani.

Aidha, Juni 2012, waandishi wa habari, wapinzani na wanaharakati 24 walihukumiwa chini ya sheria mpya ya kupambana na ugaidi. Mwandishi mmoja wa blogu alihukumiwa kifungo cha miaka 18. Utawala wa Meles unashutumiwa pia kwa kutumia fedha za misaada kwa ajili ya kampeni ya uchaguzi.

### UNDUMI LAKUWILI

Meles anayeelezwa kuwa alikuwa anapendelea kusoma, kuogelea na kucheza mpira wa tenisi katika muda wake wa mapumziko, alikuwa na kipaji cha kuzungumza mbele za watu. Kipaji hicho kinaonyesha pande mbili za kiongozi huyu. Nchini mwake alikuwa kigogo aliyezima upinzani wowote dhidi yake, ikibidi hata kwa kutumia nguvu.

Lakini katika majukwaa ya kimataifa alijionyesha kuwa msemaji na mtetezi wa Afrika, akizungumzia masuala kama vile mabadiliko ya tabianchi na athari zake kwa bara hilo.

### NI MWANAMAENDELEO

Kuna mambo ya maendeleo aliyowaletea wananchi wake katika sekta ya elimu na afya yakiwa mengi wakati wake. Kiujumla, Ethiopia ilijipatia maendeleo mengi chini ya utawala wake, licha ya kwamba mengine yalikwamishwa na ongezeko la kasi la idadi ya watu nchini humo. Hata uchumi wa Ethiopia unakua kwa haraka, lakini wanaofaidika zaidi ni viongozi wa kisiasa.

Kwa muda mwingi kulikuwapo na tetesi za kuugua kwa Meles ambaye mara kwa mara kiongozi huyo alilazimika kwenda nje ya nchi kwa matibabu. Aliposhindwa kuhudhuria mkutano mkuu wa Umoja wa Afrika uliofanyika Julai 2012 mjini Addis Ababa, ulizuka uvumi juu ya kifo chake. Hata hivyo, msemaji wake alikanusha taarifa hizo ilipofika Jumanne Agosti 12, 2012 Zenawi alifariki dunia siku hiyo ya Jumanne akiacha mke na watoto watatu. **DW**





# Wabunge wanolewa kuhusu bajeti ya mrengo wa kijinsia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP) umetoa semina kwa ajili ya kuwajengea uwezo wabunge kuandaa bajeti kwa mrengo wa kijinsia ili kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wanawake nchini.

Akiwasilisha mada katika semina hiyo, mtaalamu wa masuala ya bajeti, Gemma Akilimali, alisema kuwa bajeti yenye mlengo wa kijinsia inahitaji ili kujibu kero zinazowakabili wanawake katika maeneo mengi nchini.

Alisema kuwa bado kuna kero nyingi ambazo zinawakabili wanawake, hivyo ipo haja zipoandaliwa bajeti kuwa na mrengo wa kijinsia ili ziweze kutoa suluhu kwa makundi hayo.

Alisema wabunge wanatakiwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa bajeti inayotengwa inajibu kero ambazo zinamlengo wa kijinsia.

"Lazima inapokuja bajeti ili wabunge mpitishe lazima mjiridhishe kuwa inamrengo wa kijinsia kwa mafano kama sekta ya maji inaweza kutengwa fedha kwa ajili ya kisima cha maji, lakini maji hayo hayatoki hivyo kero kwa kundi hili inaendelea kuwepo," alisema.

Aidha, alisema pia katika masuala ya bajeti yenye mrengo wa kijinsia lazima wabunge waangalie maeneo kama sekta ya elimu, afya, maji ili kubaini kama kero zilizopo zimejibiwa. "Kuna maeneo watoto wetu wa kike wanapata tabu kutembea umbali mrefu kutokana na kukosekana kwa mabweni kwa ajili ya watoto wa kike hali inayochangia kuwapo kwa mdondoko wa wanafunzi wa kike," alisema.

Kutokana na hali hiyo, aliwaomba wabunge kuhakikisha kuwa wanakuwa makini katika uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia, ambayo itasaidia kuwaondolea wasichana kero za kutembea umbali mrefu.

Kadhalika alisema kuwa bajeti yenye mrengo wa kijinsia pia itawezesha wasichana kupata vyumba kwa ajili ya kujisitiri wanapokuwa katika hedhi.

"Kuna maeneo tumefanya nayo kazi kama vile Kishapu juu ya dhana hii ya bajeti yenye mrengo wa kijinsia katika ngazi ya halmashauri kumekuwapo na mabadiliko makubwa ikiletwa bajeti watu wanaikataa kutokana na kutokuwa na mrengo wa kijinsia," alisema.

Naye mchambuzi na mtafiti wa masuala ya kijinsia, Dk. Geofrey Chambua, alisema bajeti yenye mrengo wa kijinsia itasaidia kuondoa kero zilizo kwa wanawake.

Alisema pamoja jitihada mbalimbali zilifanywa na serikali katika sekta ya afya hasa katika kupunguza vifo vya watoto, lakini bado ipo haja ya kuwa na bajeti ya wananchi yenye mrengo wa kijinsia.

"Takwimu zinaonyesha hivi sasa tumepiga hatua katika kukomesha vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vile vya awali 556, kwa hadi 292, lakini bado tunayo kazi ya kufikia dira ya Taifa ya 2025 ya kuwa na vifo 40, kwa mwaka hivyo bajeti yenye mrengo wa kijinsia inahitajia sana waheshimiwa wabunge," alisema Dk. Chambua.

Mbunge wa Viti Maalumu, Esther Buraya, alisema bado lipo tatizo kubwa katika baadhi ya maeneo wajawazito kudaiwa fedha wakati wa kujifungua.

Alisema kutokana na hali hiyo, serikali inatakiwa kuweka msisitizo katika maeneo ambayo ni muhimu kwa wanawake na kutoa kipaumbele wakati wa kutenga bajeti.



Meneja wa Mradi wa Elimu Jumuishi Tanzania wa Kanisa la FPCT, Ibrahim Suleiman, akizungumza kwenye warsha ya mgawanyo wa majukumu kwa kamati mbalimbali, zikiwamo baraza la watoto, kikundi cha wazazi na wadau wa elimu jumuishi kutoka wilaya ya Bahi na Jiji la Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watumishi sekta ya uvuvi wafundwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka watumishi wa sekta ya uvuvi kufanya kazi kwa uadilifu, uaminifu na nidhamu ili kuleta tija katika sekta hiyo.

Waziri Ndaki aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua Baraza la Wafanyakazi Sekta ya Uvuvi.

"Viongozi wa ngazi zote tunatakiwa kusimamia na kuchukua hatua, inapotokea mambo ya kinidhamu ya watumishi na watendaji wanapokuwa yameenda sivyo lazima viongozi wa ngazi ya idara, taasisi, kitengo, wizara lazima tusimamie ipasavyo," alisema.

Alihimiza baraza hilo kusimamia ushirikishwaji wa watumishi katika utendaji kazi wa kila siku ili kupunguza manung'uniko.

"Ningependa kusisitiza juu ya umuhimu wa ushirikishwaji wa watumishi katika ufanyaji kazi katika vitengo vyote, sisi wote tunajua ushirikishwaji ni jambo la msingi mahali pa kazi, hasa kwenye mambo yanayohusiana na hizo idara na taasisi na vitengo vyetu tukiwashirikisha wafanyakazi tutapunguza manung'uniko," alisema.

Aliongeza: "Maana kama kuna jambo kubwa tunaliamua tunalipitisha, basi wakati wa utekelezaji hatulaumiani sana kwa sababu wote tumehusika na tumeshirikishwa."

Aliwataka viongozi wa baraza hilo kusimamia nidhamu pamoja na kuchukua hatua pindi yanapotokea mambo ya ukosefu wa nidhamu mahala pa kazi.

"Niwaombe sana ndugu wajumbe masuala ya uadilifu, uaminifu, nidhamu kazini ni masuala ya msingi sana uzuri ni kwamba kuna sheria na taratibu na kanuni zinazotuongoza katika mambo haya, kwa hiyo tunapaswa kuziangalia na kuziheshimu ili kwamba tuweze kutoa huduma kwa wananchi wakati kwa kadri tunavyotegemewa.

"Mimi pia kama waziri ambaye nasimamia shughuli za uendeshaji na utendaji kazi wa kila siku wa wizara haitoshi tu kwamba mimi sihusiki na masuala ya kinidhamu ya kimaadili na uadilifu lakini natakiwa kuhakikisha kwamba wizara kwa ujumla inaendana na masuala ya nidhamu kazini inaendana na masuala ya uadilifu na uaminifu kazini," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza hilo ambaye ni Katibu Mkuu anayeshughulikia uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema kikao hicho kitakuwa na agenda za wajibu wa mwajiri na taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21 na mpango wa bajeti kwa mwaka 2021/22.

# Watendaji waagizwa kuweka mkakati wa kutatua kero za jamii

**Na Auguta Njoji,** DODOMA

WATENDAJI wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii wametakiwa kuweka mkakati wa kutatua kero za jamii ikiwamo ndoa za utotoni na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, alitoa kauli hiyo alipokuwa akifungua baraza la wafanyakazi wa idara hiyo, katika ukumbi wa Makao ya Taifa ya Watoto ya Kikombo.

Aidha, alimwagiza Katibu Mkuu wa idara hiyo, Dk. John Jingu, kutumia wataalamu wake kusimamia majukumu ya wizara na kuhakikisha watumishi wanafanya kazi kwa weledi.

Alisema wizara inatakiwa kuwatumia ipasavyo watumishi wake katika kuhakikisha mipango iliyowekwa inasimamiwa na kutekelezwa kikamilifu ili kuboresha huduma za wizara hiyo na kutatua kero mbalimbali katika jamii.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Dk. Jingu alisema lengo la baraza hilo ni kushirikiana watumishi katika mipango na utekelezaji wa majukumu ya wizara.

Jingu alisisitiza kuwa vikao vya baraza hilo ni kiunganishi muhimu cha kuiwezesha menejimenti na watumishi kufanya kazi kwa weledi na kuondokana na dukuduku miongoni mwa wafanyakazi.

Aliwahimiza wafanyakazi wenye hoja kuziwasilisha katika mamlaka ili zipatiwe ufumbuzi.

"Pale penye hoja kama madeni na stahiki mbalimbali leteni, tufanye tuhakiki na kulipa madeni na stahili mbalimbali," alisema.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo alitembelea watoto waishio katika makao ya Taifa ya kulelea watoto wenye mazingira magumu kikombo na kutoa zawadi kwa ajili ya sikukuu ya Eid El Fitr.

Alisema zawadi hiyo imetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwawezesha watoto hao kusherehekea siku hiyo kwa furaha kama ilivyo kwa familia zingine.

Akizungumza baada ya kupokea zawadi hizo, Mkuu wa Makao hayo, Tullo Masanja, alimshukuru Rais Samia kwa kuwakumbuka watoto hao.

**Aidha, alimwagiza Katibu Mkuu wa idara hiyo, Dk. John Jingu, kutumia wataalamu wake kusimamia majukumu ya wizara na kuhakikisha watumishi wanafanya kazi kwa weledi.**





# RC kufikisha malalamiko ya madiwani ubadhirifu fedha

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Nicodemas Mwangela, ameahidi kufikisha malalamiko yaliyotolewa na madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kwenye ngazi kuu ya kitaifa juu ya matumizi mabaya ya madaraka, ubadhirifu wa fedha unaodaiwa kufanywa na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Hanji Godigodi.

Mwangela alitoa kauli hiyo jana wakati akifunga kikao maalum cha Baraza la Madiwani alichokiitisha kwa lengo la kusikiliza malalamiko na majibu ya Mkurugenzi kutokana na tuhuma zilizoelekezwa dhidi yake.

Alisema hoja na malalamiko yaliyotolewa na madiwani amezipokea kwa sababu yeye sio mwenye uamuzi wa mwisho atafikisha kwenye ngazi ya juu ili kupata ufumbuzi kwa masuala hayo. Aliwaomba madiwani kuendelea kumpatia ushirikiano mkurugenzi huyo, wakisubiri uamuzi wa Serikali Kuu kwa kuhakikisha wanasimamia na kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Hanji Godigodi, aliwaomba radhi madiwani kwa mambo mbalimbali aliyotuhumiwa kuyafanya na kuahidi kutorudia tena.

Alisema Baraza la Madiwani lilimtaka kujibu hoja tisa ambazo zilihusu usimamizi wa miradi na alifanikiwa kuzitolea ufafanuzi licha ya kukiri pia kuwa taarifa ya hoja hizo haikukamilika.

“Nawaomba radhi madiwani wote wa Halmashauri ya Mbozi kwa mambo yote niliyoyafanya mimi ni binadamu nina mapungufu naahidi kubadilika na kutorudia tena, kikubwa tuendelee kushirikiana,” alisema Godigodi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, George Msyani, alisema wakati wanaendelea kusubiri uamuzi kutoka kwa viongozi wa juu wa kitaifa ni muhimu sasa kuendelea kushirikiana ili kuongeza makusanyo kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato.

Alisema wilaya hiyo ina vyanzo vingi vya mapato, lakini tatizo fedha zinazokusanywa ni ndogo na aliagiza usimamizi zaidi kwa kuwaomba maofisa wanaosimamia ukusanyaji kuwa wazalendo.

Awali, madiwani hao wakati wakichangia hoja, walidai kuwa Mkurugenzi aliwahi kuandika bango la kupiga marufuku madiwani kuingia kwenye ofisi yake.

Kauli hiyo ilithibitishwa na Diwani wa Bara, Aloyce Mdalavuma aliyedai Mkurugenzi amekuwa na manyanyaso kwa watumishi hali iliyosababisha pia kuweka bango katika ofisi yake kuzuia madiwani kutokanyaga ofisini kwake waraka ambao pia ulimfikia Makamu Mwenyekiti wa halmashauri kwa wakati huo.

Diwani wa Itumpi, Samson Nzunda, alisema watumishi wa halmashauri wanahusika na ubadhirifu wa fedha za miradi na kuhitaji TAKUKURU kuingilia kati na kwamba yuko tayari kutoa ushirikiano atakapohitajika kwa kuwa anawafahamu.

Diwani wa Nyimbili, Tinson Nzunda, aliliambia Baraza hilo kuwa miongoni mwa masuala yanayomkabili Mkurugenzi huyo ni matumizi mabaya ya fedha zinazotokana na makusanyo ya kahawa Sh. milioni 187.

Alisema baada ya kubaini usimamizi mbovu wa makusanyo, walimshauri mkurugenzi kuunda kikosi kazi cha kufuatilia, lakini aligoma kutoa ushirikiano na kuamua madiwani kujitolea kwa gharama zao kufuatilia na kubaini kiasi hicho cha fedha kingeweza kupotea.



Gari maalum la kunyanyua magari ‘Break Down’ likijiandaa kulinyanyua lori la mizigo lililoanguka katika eneo la kona za Mwambegele, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya juzi. PICHA: NEBART MSOKWA

# Zaidi ya watu 4,000 wafanyiwa ukatili Mbarali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WATU 4,223 wamefanyiwa ukatili wa aina mbalimbali katika Wilaya ya Mbarali katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015 mpaka 2020 hali ambayo inadaiwa kutishia ustawi wa wananchi wa wilaya hiyo.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa wilaya hiyo, David Makere, alisema hayo katika Kata ya Madibila wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kupinga ukatili wa kijinia na uhifadhi wa vyanzo vya maji inayofanywa na shirika lisilokuwa la kiserikali la Save Life Organization of Tanzania (SALIOTA).

Alisema watu hao waliofanyiwa ukatili na kutoa taarifa kwenye mamlaka mbalimbali, wanawake ndio waliokuwa wengi zaidi ikilinganishwa na wanaume.

Alisema wanawake walikuwa 3,449 huku wanaume wakiwa 774 na taarifa za ukatili huo zilikuwa zinaripotiwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, polisi, ofisi za ustawi wa jamii na kwa maofisa maendeleo ya jamii pamoja na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali.

“Ili kukabiliana na tatizo hili tumekuwa tukitoa elimu kwa jamii ili tusaidiane kukabiliana na tatizo hili kwa sasa tumeshatoa elimu ya kukabiliana na tatizo hili la ukatili kwa walimu wakuu na walimu wanasihi na tunaendelea kutoa elimu kwa makundi mengine,” alisema Makere.

Ilisema idadi ya taarifa za ukatili ambazo zimekuwa zikitolewa zimekuwa zikitofautiana mwaka hadi mwaka na mwaka 2018 idadi ya taarifa ilikuwa kubwa kuliko miaka yote kwa kuwa na taarifa 946.

Mkurugenzi wa Shirika la SALIOTA, Elisha Mwanikawage, alisema lengo la shirika hilo ni kuhakikisha ukatili wa kijinsia hasa kwa wanawake na watoto katika wilaya hiyo ikiwamo kuweka usawa wa upatikanaji wa huduma za kijamii kwa usawa.

Alisema watahakikisha kunakuwapo na usawa wa upatikanaji wa elimu kwa watoto wa kike na wa kiume, upatikanaji wa huduma za afya pamoja na upatikanaji wa maji.

Alisema vilevile watahakikisha wanakomesha ukataji ovyo wa miti pamoja na uchomaji wa misitu ya asili na isiyokuwa ya asili ili kulinda mazingira.

“Tutahakikisha pia tunakemea ujangili wa wanyamapori walioko ndani ya hifadhi za taifa na kwenye mapori tengefu ili tuhakikishe hawa wanyama wanakuwa na faida kwa vizazi vya sasa na vya baadaye,” alisema Mwanikawage.

Akizindua kampeni hiyo, Mbunge wa Viti Maalumu kupitia Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi Taifa, Bahati Ndingo, aliwataka wadau hao kuhakikisha wanafikisha elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia maeneo ya vijijini kwa kuwa maeneo hayo ndiyo yenye tatizo kubwa zaidi.

Alisema moja kati ya vyanzo vya ukatili wa kijinsia kwenye jamii ni imani potofu miongoni mwa wananchi hasa vijijini ambako elimu ni ndogo kuhusu ukatili.

Alilipongeza Shirika la SALIOTA kwa kuanzisha kampeni hiyo kwa maelezo kutasaidia kutokomeza ukatili pamoja na kuyalinda mazingira katika wilaya hiyo.

# Viongozi watakiwa kuiga mfano wa Rais Samia

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WATUMISHI wa umma wa ngazi mbalimbali za uongozi nchini, wametakiwa kuiga uadilifu wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kiongozi huyo hajawahi kutuhumiwa mahali kwa ufisadi licha ya kutumikia taifa kwa muda mrefu kwenye nyadhifa mbalimbali.

Kauli hiyo ilitolewa juzi wilayani Kyela na Askofu Mkuu wa Kanisa la Assemblies of God Tanzania (TAG), Dk. Barnabas Mtokambali, wakati wa ibada maalum ya kuweka wakifu viongozi wapya wa kanisa hilo Jimbo la Mbeya Kusini.

Alisema hakuna mahali popote zimewahi kusikika tetesi za Rais Samia kutokuwa mwadilifu kwenye uongozi hali inayowafanya Watanzania kutokuwa na wasiwasi na uongozi wake.

“Hatujasikia minong’ono ya siri wala ya wazi kwamba kiongozi huyu ni fisadi ama ni mla rushwa, kwa hiyo ni vizuri sana viongozi wengine wa serikali wakaiga mfano wake kwa kuepuka rushwa na matumizi mabaya ya madaraka,” alisema Mtokambali.

Alisema uadilifu wa Rais Samia ndio uliomfanya ateuliwe na aliyekuwa rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli, amteue kuwa mgombea mwenza kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2015 na wa 2020.

Aliwataka viongozi wenzake wa dini wakiwamo waliosimika wakfu kwenye jimbo hilo kuisaidia serikali kwa kukemea mambo maovu kwenye jamii ili taifa liendelee.

Alisema viongozi wa dini wataendelea kuiunga mkono serikali kwa kukemea mambo mabaya yanayofanyika kwenye jamii huku akisisitiza kuwa wataendelea kuwaombea viongozi wa serikali ili waliongoze taifa kwenye miongozo inayotakiwa.

Katika ibada hiyo, Dk. Mtokambali alimweka wakifu, Meshaki Njowela kuwa Askofu mpya wa kanisa hilo Jimbo la Mbeya Kusini akimrithi Askofu Daison Ipambalaga.

Wakizungumza wakati wa ibada hiyo, baadhi ya maaskofu wa kanisa hilo waliwaomba waumini na madhehebu mengine kushikamana ndani na nje ya makanisa yao ili kudumisha amani ya nchi.

Askofu aliyemaliza muda wake, Ipambalaga aliahidi kuendelea kushirikiana na Njowela kuwaongoza waumini wa kanisa hilo ili kuhakikisha waumini hao wanaendelea kuwa wamoja.

Alisema alikubali kumkabidhi mwenzake nafasi hiyo kwa amani na ndiyo maana ataendelea kushirikiana naye kwenye uongozi ikiwa ni pamoja na kumwongoza kwenye baadhi ya vitu ambavyo vitakuwa vigeni kwake.

“Hii kazi ni ngumu sana, lakini tunaifanya kwa moyo wote kutokana na kwamba ni kazi ya Mungu, wakati mwingine huwa inatufanya tusilale usingizi, hivyo nakuomba ndugu yangu Njowela uwe mvumilivu kwenye kazi hii,” alisema.

Naye Askofu, Njowela alisema ana uzoefu kwenye kazi hiyo kutokana na muda wote ambao Ipambalaga alikuwa Askofu yeye alikuwa msaidizi wake.

# Mtambo wakwamisha mjadala barazani

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wamekwama kujadili makadirio na matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais (Uchumi na Uwezeshaji) ya mwaka wa fedha 2021/2022, baada ya mtambo wa vipaza sauti kuharibika.

Uamuzi wa kuahirisha kikao ulitangazwa jana na Mwenyekiti wa Baraza Mwanaasha, Khamis Juma, muda mfupi baada ya kuingia katika ukumbi wakati wajumbe wakijiandaa na kipindi cha maswali na majibu asubuhi wakiwa katika utulivu.

"Waheshimiwa wajumbe, kutokana na tatizo la mitambo yetu ya vipaza sauti kuwa na tatizo, naahirisha kikao mpaka kesho asubuhi," alisema Mwanaasha na wasaidizi wake kuanza kunyanyua sifa ya baraza na kutoka nje ya ukumbi. Akizungumzia na Nipashe kuhusu tatizo hilo, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Raya Issa Mselem, alisema mtambo wa vipaza sauti unakabiliwa na matatizo ya kiufundi, lakini juhudi za kutafuta vifaa kutoka nje ya nchi zinaendelea kufanyika.

"Tumeagiza vifaa Uingereza, lakini upatikanaji wake bado mgumu, tunaendelea kutafuta ili kuondoa tatizo la vipaza sauti kuharibika." alisema Raya, lakini hakufafanua mtambo huo ulitengenezwa mwaka gani na kikomo cha matumizi.

Alisema mafundi wanaendelea kurekebisha matatizo yaliyojitokeza ili wajumbe waweze kuendelea kama kawaida na vikao vya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, ingawa hakufafanua kuhusu malipo ya posho za wajumbe kwa siku hiyo baada ya kikao kutokufanyika.

Tatizo la Baraza la Wawakilishi kuahirisha vikao kutokana kuharibika kwa mfumo wa mtambo wa vipaza sauti, limekuwa la kawaida kujitokeza, ingawa mafundi wamekuwa wakifanya jitihada za kurekebisha kwa wakati.

Baada ya kikao kuahirishwa, baadaye Kamati ya Kudumu ya Uongozi ya Baraza la Wawakilishi ilikutana, lakini haikufahamika ajenda ya kikao hicho.



Mwakilishi wa Jimbo la Mwera, Mihayo Juma Nhunga (kushoto), akijadiliana jambo na Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni, Miraji Kwanza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Sababu za kufungwa vituo vidogo vya polisi zatajwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UHABA wa askari wa Jeshi la Polisi umesababisha kufungwa kwa baadhi ya vituo vidogo vya jeshi hilo vilivyopo mjini na nje ya Mji wa Zanzibar.

Hayo yalisemwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said, aliyetaka kujua sababu za kufungwa kwa vituo vya polisi.

Dk. Mohamed alizitaja sababu za msingi za kufungwa kwa vituo hivyo ni uhaba wa askari wa Jeshi la Polisi unaowakabili kwa sasa, ambao umechangiwa kwa kiasi kikubwa kwa muda mrefu jeshi hilo kutotoa ajira za kujaza nafasi ya askari waliostaafu na walioacha kazi.

Alivitaja vituo vidogo vya Jeshi la Polisi vilivyofungwa au vengine hufunguliwa kuanzia asubuhi na kufungwa jioni, ikiwamo Mlandege, Malindi na Muembe Mchomeke.

Hata hivyo, alisema baadhi ya vituo hufunguliwa kwa kadri ya hali halisi ilivyo kwa mfano, katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, baadhi ya vituo vinafanya kazi kwa ajili ya kuweka usalama na ulinzi wa mali za wananchi kutokana na kuwapo kwa mzunguko mkubwa wa wananchi.

"Mheshimiwa Spika, napenda kukiri kwamba baadhi ya vituo vya Jeshi la Polisi vilivyopo maeneo mbalimbali ya mjini na nje ya mji vimefungwa, kwa sababu mbalimbali ikiwamo uhaba wa askari wa kufanya kazi, ingawa baadhi ya wakati vituo vinafunguliwa kutokana na mahitaji halisi," alisema.

## SMZ yaeleza mchango wa wanaoishi nje

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema wananchi wameanza kuona matunda na mchango wa Diaspora kwa ajili ya shughuli za maendeleo na kukuza uchumi, baada ya serikali kupitisha sera yake mwaka 2017.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Kazi, Uchumi na Uwekezaji), Mudrik Ramadhan Soraga, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Alisema serikali baada ya kufanikiwa kutayarisha sera ya Diaspora ya mwaka 2017 na sheria nambari 4 ya mwaka 2020 inayohusu mambo ya Diaspora, matunda yake yameonekana ikiwamo upatikanaji wa huduma za kijamii, maendeleo na kiuchumi kwa wananchi wa Zanzibar.

Alieleza kuwa Wazanzibari waliopo nje ya nchi wamekuwa mstari wa mbele katika kusaidia maendeleo ya sekta ya elimu, afya na upatikanaji wa huduma za majisafi vijijini.

Alisema wana waliopo nje ya nchi wamesaidia miradi ya upatikanaji wa huduma za majisafi na salama katika visiwa vidogo vilivyopo Pemba ikiwamo Kisiwa Panza na Uvinje katika usambazaji wa huduma ya majisafi na salama na ujenzi wa madarasa.

"Sera ya Diaspora ya mwaka 2017 pamoja na sheria namba 4 ya wanadiaspora na wananchi kwa ujumla matunda yake tumeanza kuyaona, ambapo tumefanikiwa kuwaunganisha kwa kuwatambua wote waliopo katika mabara yote duniani," alisema.

Soraga aliwataja wana Diaspora waliojitokeza na kutambuliwa rasmi ni kutoka nchi za Skandinavia zikiwamo Denmark, Sweden, Finland na Uholanzi.

Nchi nyingine ambazo wana Diaspora wake wametambuliwa ni Uingereza, Marekani, India na Afrika Kusini.

**"Sera ya Diaspora ya mwaka 2017 pamoja na sheria namba 4 ya wanadiaspora na wananchi kwa ujumla matunda yake tumeanza kuyaona, ambapo tumefanikiwa kuwaunganisha kwa kuwatambua wote waliopo katika mabara yote duniani," alisema.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## CLASSFIED-LA ACCAPILLA INN INAUZWA

**LA ACCAPILLA INN INAUZWA IPO MBANDE - MSONGOLA: Ina Lodge mpya ya Kisasa yenye Vyumba 9 vyote Self Contained, Bar yenye Kaunta 2 chini na juu, Club ya ndani, Ukumbi na Kisima cha Maji cha Kisasa. Ukubwa wa eneo SQM 2000. Bei 300/= Milioni tu. TANLANDS REAL ESTATE AGENCY SIMU NO: 0628 336736 / 0652 032980**

***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa***
***Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGZAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA TARAKA: 51/2021**

**MADAI/MUOMBAJI/MSIMAMIZI: JOYCE JUVENALIS**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: AMANI RONALD MAKYARA**

**KWA: AMANI R. MAKYARA**
**WA MOSHI KIDIA**

**OMBI LA MDAI/MUOMBAJI/MSIMAMIZI JOYCE JUVENALIS**
**MADAI YA : TALAKA**

Unatakiwa kuhudhuria hapa mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa . Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 19 mwezi 5 mwaka 2021 saa 2:30 Asubuhi.
Angalia kama *kuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 11 mwezi 5 mwaka 2021

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISC.CIVIL APPLICATION NO.346 OF 2020**
**(from the judgment of civil appeal no 28 of 2018 before Hon. Ebrahim, J delivered on 26/6/2020, originating from kinondoni district court in civil case)**
**DOREEN PONDAMALI……………....APPLICANT**
**VERSUS**
**LATIFAMULIKA…………………......RESPONDENT**
**SUMMONS FOR PUBLICATION**
**TO:**
**LATIFA MULIKA**
**P O BOX**
**DA ES SALAAM**

**WHEREAS**, the above mentioned case has been fixed for mention 31st day of May, 2021 at 9:00 am before **Hon Dr J.L.MASABO** –judge you are required to appear in this court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that aforementioned, the suit will be heard and determine in your absence.
**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of court this 5th day of April, 2021.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 150 CJX – BOXER. CHASSIS NAMBA MDZAZIBY9KWF99646. ENGINE NAMBA PFZWKF30534. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: DAR/MAG/RB/241502/2021.

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTRHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA 17 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**MKEJINA ATHUMANI MABUKU**
**@MKEJINA-MAREHEMU ATHUMANI SEBUNGE**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**SALEHE RASHID MSAGATI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 27th mwezi wa MAY 2021.
Imewasilishwa Dar Es Salaam leo tarehe 29th mwezi **APRIL 2021**

NAIBU MSAJILI

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**JUSTIN ADAM NSHINSHI** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 884 AWP,** Toyota Hilux. Engine namba: **3L14299251.** Chasis namba: **LN 46007107** Kwa yeyote atakayeiona anaombwa aripoti kituo chochote cha polisi kwa: **MBE/MBE/R-B/211480/2021**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 30 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**MOHAMED ABDALLAH WALLI DAYA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**SULTANA MOHAMED ABDALLAH WALLI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 16 Mwezi wa 06, 2021. Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 27 Mwezi wa 04, 2021.

NAIBU MSAJILI

OFISI ZA MATANGAZO
Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam.
Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
website: www.ippmedia.com

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI**
**INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM. MOB:**
**+255 - 0782253676**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

## Serikali yatangaza kupanda bei ya pamba

**Na Happy Severin,** BUSEGA

SERIKALI imetangaza kupanda kwa bei ya pamba katika msimu mpya wa ununuzi 2020/21, kuwa Sh. 1,050 kwa daraja la kwanza.

Aidha kwa daraja la pili kilo moja itanunuliwa kwa Sh. 525.

Bei hiyo mpya imetangazwa jana ikiwa ni ongezekezo la Sh. 240 lililotangazwa mwaka jana msimu wa 2019/20 iliyokuwa Sh. 810 kwa kilo moja.

Akitangaza bei hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, Mkuu wa Wilaya ya Busega, Tano Mwera, alisema kuwa licha ya bei kupanda bado tija imekuwa ndogo kwenye zao hilo.

Mwera alisema kuwa katika msimu wa mwaka huu, uzalishaji wa pamba umeongezeka kutoka tani 122,650 mwaka 2019/20 na kufikia tani 393,000 msimu wa 2020/21 ongezekezo la asilimia 68 ya uzalishaji na Mkoa wa Simiyu umezalisha tani 141,095.

Aliitaka bodi ya pamba kushirikiana na mahakama, kuanzisha mahakama inayotembea ili kuwachukulia hatua kali watakaobainika kuchezea mizani kwa lengo la kuwaibia wakulima.

Awali, akizungumza kwenye hafla hiyo Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba, Marko Mtunga, alisema licha ya serikali kutoa elimu kwa wakulima kufuata kanuni bora za kilimo, bado eneo la kupanda kwa mstari limekuwa changamoto kubwa kwa wakulima.

Aliwataka wadau wa zao hilo kuhamasisha wakulima kujiunga na AMCOS kutatua changamoto zinazowakabili. Joshua Emmanuel, mmoja wa wakulima alishukuru kwa ongezeko la bei, hata hivyo, alisema halijaleta matumaini kwa wakulima wengi kutokana na kutumia gharama kubwa katika uzalishaji.

Naye Katibu wa chama cha wanunuzi wa pamba nchini, Boaz Ogolla, alisema wanunuzi wako tayari kununua pamba yote waliyozalisha wakulima kwa kuwa uwezo upo na uhitaji ni mkubwa kwenye viwanda vyao.

# Waziri aipa neno WHO kuhusu chanjo ya corona

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amesema chanjo ya corona ni muhimu, lakini kinachotakiwa ni kwa Shirika la Afya Duniani (WHO) lisaidie kuleta imani kwa wananchi, kwamba chanzo hizo zitasaidia bila kuleta madhara kwa watakaoitumia.

Alitoa msimamo huo katika kipindi cha dakika 45 kinachorushwa na luninga ya ITV, baada ya kuulizwa msimamo wa Tanzania kuhusu chanjo ya corona ambayo WHO ilisisitiza kila nchi iweze kuipata ili kupunguza vifo vinavyotokana na corona.

"Chanjo ni muhimu sana na ndio maana kila mtu anapenda kumpeleka mtoto wake kupata chanjo, WHO wasiende kwenye majukwaa na kusema chanjo ni muhimu, kinachotakiwa watusaidie kutupa imani kwamba chanjo hizi zitatusaidia bila kutuletea madhara," alisema.

Balozi Mulamula alisema kwa kuwa WHO ndio inayoratibu chanjo hii na ina wataalamu, kuna umuhimu kuunda hata task force (kikosi kazi) nchini ili kupata chanjo ambayo itatulinda, badala ya kutoa maagizo tu.

"Sihoji hata mara moja kuhusu umuhimu wa chanjo, lakini cha msingi tupate chanjo ambayo itatulinda kwa kutumia wataalamu wa WHO, tunataka kuona chanjo ambayo imeidhinishwa na WHO ndiyo itumike, tusiyaachie makampuni," alisema.

Balozi Mulamula alisema Tanzania yupo mwakilishi wa WHO, lakini anawashirikisha vipi wataalamu wa nchini badala ya kuendelea kusema Tanzania imejitenga katika chanjo hii, wakati hakuna jitihada zilizochukuliwa na shirika hilo.

Alisema Tanzania siyo kwamba inazuia chanjo, ndio maana katika Umoja wa Afrika tunatakiwa tuwe na chanjo yetu ya uhakika, ambapo wataalamu wanatakiwa wasaidie katika hili, na kwamba suala hili lisiingie siasa bali waachiwe wataalamu wafanye kazi yao.

Balozi Mulamula alisema janga la corona bado ni changamoto katika nyanja ya kimataifa ambapo nchi ndogo na kubwa zote zimeathirika, na hata baada ya kupatikana chanjo, bado kuna mkanganyiko kama italeta majibu hasa ikizingatia imeanza kuleta madhara katika baadhi ya nchi.

Alisema Umoja wa Afrika umejipanga katika janga hili la corona ambapo zimeundwa 'task force' mbili, moja ikihusika na janga la corona kwa ujumla kwa kutafuta fedha na nyingine ikishughulikia suala la chanjo ili kuwapo uratibu mzuri, ambao utaendana na mazingira ya nchi za Afrika.

"Kimsingi hakuna nchi inayoweza kusimama pekee yake na sisi kama Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, jukumu letu kubwa ni kuangalia ni namna gani tutashirikiana na nchi zote katika janga la corona kwani hakuna nchi yenye jawabu, kila nchi inajaribu kuona jinsi itakavyookoa wananchi wake," alisema.




Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu (mwenye miwani), akikabidhi msaada wa vyakula kwa mlezi wa kituo cha kulelea watoto yatima cha New Faraja Orphanage cha Mburahati, jijini Dar es Salaam, ili kuwawezesha kufurahia Sikukuu ya Eid El-Fitr, kama watoto wengine waliopo majumbani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoto wapewa zawadi Sikukuu ya Eid El Fitr

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim imetoa msaada wa vyakula kwenye vituo vinne vya kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu vya Dar es Salaam, Mbeya, Shinyanga na Karatu.

Lengo ni kuwawezesha watoto hao waweze kusherehekea vizuri sikukuu ya Eid El Fitr.

Msaada huo ulikabidhiwa na viongozi waandamizi wa benki hiyo wakiwa wameambatana na wafanyakazi wengine na ulihusisha mahitaji muhimu ikiwamo mchele, mafuta ya kupikia, sukari, unga wa sembe, unga wa ngano, maharage pamoja na katoni za juisi na maji ya kunywa.

Akiwasilisha msaada huo katika kituo cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu cha New Faraja Orphanage Centre kilichopo Mburahati Dar es Salaam, Meneja Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu, alisema imekuwa ni utaratibu wa benki hiyo kusaidia makundi na taasisi mbalimbali kupitia mpango wake wa uwajibikaji kwa jamii unaofahamika kwa jina "Exim Cares".

"Msaada huu ni maalum kwa ajili ya kusherehekea sikukuu ya Eid El Fitr, na ni mwendelezo wa utaratibu wetu wa kile ambacho tumekuwa tukikifanya kila mwaka ambapo wafanyakazi wa benki ya Exim pamoja na uongozi kwa ujumla tumekuwa tukiguswa kuhakikisha kwamba watoto wanaoishi kwenye vituo hivi wanafurahia Sikukuu hizi kama wenzao waliopo majumbani," alisema.

Kafu alivitaja vituo vingine ambavyo vimekabidhiwa msaada huo ni cha watoto yatima cha Nuru kilichopo jijini Mbeya, Kituo cha Shinyanga Society kilichopo mkoani Shinyanga na Kituo cha Shalom kilichopo wilayani Karatu.

Kafu alitoa wito kwa watoto hao kuhakikisha wanasoma kwa bidii huku wakitanguliza nidhamu kwenye kila jambo wanalofanya ikiwamo masomo na shughuli zao za kila siku wawapo shuleni na kituoni hapo.

Wawakilishi wa vituo hivyo waliishukuru benki hiyo kwa uamuzi wake wa kuwakumbuka watoto yatima ili nao waweze kusherehekea vizuri sikukuu ya Eid El Fitr kama ilivyo kwa familia nyingine.




# SPORTPESA YAJIVUNIA MIAKA 4 MLIMA WA MAENDELEO TZ

Wachezaji wa Simba wakiwa na wenzao wa Sevilla kutoka Hispania. **Chini;** kikosi cha Everton ya England kilipokuja nchini mwaka 2017. **NA MPIGAPICHA WETU**




**Na Mwandishi Maalum**

MEI 10, mwaka huu, kampuni maarufu zaidi ya michezo ya kubashiri nchini ya SportPesa imetimiza miaka minne ya utendaji kazi hapa nchini.

Kwa sasa, SportPesa ndio kampuni maarufu zaidi nchini katika zile zinazojihusisha na mchezo wa kubahatisha na kuna mengi wameyafanya katika kipindi cha miaka minne tu nchini, na kuwa gumzo kuliko kampuni nyingine.

Unaweza kusema si kazi nyepesi kusema kwamba wamefika hapo haraka sana kwa kujijengea heshima kubwa na mafanikio ya juu ndani ya kipindi kifupi cha miaka minne tu.

Wakati mwingine si vizuri kujisifia, lakini kama wangepata nafasi ungeweza kuwaambia SportPesa wana haki ya kujisifia kwa kuwa wamefanya makubwa na hasa katika jamii ya Watanzania.

Jamii ya wanamichezo na hasa ya mchezo wa soka inaweza kuwa shahidi namba moja wa SportPesa, kwamba wamefanya makubwa na kuchangia kwa ukubwa sana maendeleo ya jamii ya wanamichezo.

**YANGA NA SIMBA**

Kama unakumbuka, si mbali sana, Aprili mwaka 2017 ndio kipindi SportPesa walitangaza kuingia mkataba na klabu kubwa mbili za Yanga na Simba. Ulikuwa mkataba mnono wa miaka mitano wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 10 kwa kuwa kila timu ingepata kwa kuanzia mwaka wa kwanza takribani Sh. bilioni moja na baada ya hapo ikawa inachukua zaidi ya bilioni kila moja, si jambo dogo.

Huu ndio udhamini mkubwa zaidi kwa Yanga na Simba tangu zilizoanzishwa mwaka 1935 na 1936. Udhamini ambao wengi hawakuamini kama unaweza kufanyika na ukaendelea. Sasa umebakiza mwaka mmoja tu kumalizika, huku wengi wakitega masikio kuhusiana na wakombozi hao wa Yanga na Simba, wanaingia mkataba huu kwa muda gani tena ili kuendeleza mapinduzi ya soka kupitia wadau wa mchezo huo SportPesa.

**SINGIDA UNITED:**

Wengi waliamini SportPesa ingeweza kuishia kwa Yanga na Simba kwa kuwa ilimwaga kiasi kikubwa cha fedha kwa wakongwe hao. Lakini bado SportPesa ikaendeleza udhamini tena, safari ikishuka kwa timu nyingine kama Singida United ambayo wakati huo ilikuwa katika Ligi Kuu Bara na ikawa timu ya kwanza kutoka nje ya mkoa wa Dar es Salaam kudhaminiwa na kampuni hiyo.

Wakati huo, Singida United ikawa moja ya mfano wa kuigwa.

**NAMUNGO FC:**

SportPesa haikuishia hapo, hata baada ya kuachana na Singida United, baadaye walionyesha kwamba wana nia ya kuendelea kusaidia michezo na soka walijikita hasa baada ya kumwaga mamilioni mengine ya fedha kwa Namungo FC ambayo nayo ilionyesha mchango wa SportPesa una manufaa makubwa.

Manufaa hayo ni pamoja na Namungo FC kufuzu kucheza Kombe la Shirikisho la Caf. Ikawa si kushiriki tu, badala yake ikapambana na kufikia hadi hatua makundi na kuandika rekodi mpya ya aina yake.

Ndani ya Namungo FC, SportPesa ilikuwa sehemu ya mafanikio hayo na unaona katika msimu mmoja, SportPesa ikawa mdhamini ambaye anadhamini timu mbili kutoka nchi moja zilizofanikiwa kuingia hatua ya makundi katika Kombe la Shirikisho Afrika na Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo ni Simba, si jambo dogo.

Mkataba wa Yanga na Simba kwa SportPesa umebakiza mwaka mmoja tu na miaka minne iliyopita, inaonyesha kiasi gani imechangia mabadiliko makubwa katika michezo nchini.

Soka limefaidika zaidi, limeingia katika mabadiliko makubwa ambayo yanaufanya mchezo huo kuingia kwenye rekodi mpya na mafanikio makubwa, mfano chini ya SportPesa, Simba inakwenda robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mara mbili ndani ya misimu mitatu, si mchezo.

**SPORTPESA SUPER CUP:**

Utaona mafanikio makubwa ya udhamini wa SportPesa kwa klabu nne tulizozitaja na hatua kubwa iliyofikiwa lakini hiyo haitoshi, SportPesa iliandaa mashindano makubwa ya SportPesa Super Cup.

Mara moja ikiwa jijini Dar es Salaam na mara nyingine katika mji wa Nakuru nchini Kenya na kote mambo yakaenda kwa mafanikio makubwa. Utaona ushiriki wa timu, si za Tanzania tu lakini Kenya pia hata zile zisizodhaminiwa na wao SportPesa, maana yake walichokuwa wakiangalia ni kukua kwa mchezo wa soka.

Utaona michuano ya SportPesa Super Cup iliwashirikisha JKU ya Zanzibar, mingine ikawashirikisha pia Mbao FC ya Mwanza, lengo likuwa ni kuunga mkono maendeleo ya mpira wa Tanzania hadi visiwani Zanzibar.

**EVERTON NA SEVILLA:**

Udhamini mabadiliko makubwa katika ukuaji wa soka nchini, SportPesa ikiendelea kumwaga mamilioni kuchangia. Utaona mwenyewe, yako makampuni kibao lakini hayakuwahi kurudisha namna hii kwa jamii na kuna machache yalifanya vitu kadhaa yakiiga mfano mzuri wa SportPesa.

Ukiachana na udhamini na kuandaa michuano hiyo, SportPesa iliweka rekodi nyingine kubwa kuileta timu ya Everton FC yenye rekodi kubwa ya aina yake katika soka la England, ikiwa moja ya timu mwanzilishi wa ligi hiyo.

Everton FC kutoka jijini Liverpool ikiongozwa na nyota Wayne Rooney, ilitua nchini na kucheza na Gor Mahia ya Kenya waliokuwa mabingwa wa SportPesa Super Cup mwaka 2017 na wapenda soka nchini ndio waliofaidika zaidi kwa nafasi hiyo kubwa na ya aina yake.

Acha hiyo, mabingwa mara nyingi zaidi wa Europa Cup, Sevilla kutoka Hispania, nao walitua nchini mwaka 2019 na kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya mabingwa mfululizo Simba, mechi iliyokuwa na burudani kubwa na aina yake.

Unawezaje kupata nafasi ya kuiona timu inayoshiriki EPL, ligi maarufu duniani au Sevilla kutoka La Liga, moja ya ligi bora zaidi duniani, timu zake zikicheza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam (wakati huo wa Uwanja wa Taifa), kama si SportPesa?

**NYASI ZA KISASA:**

Moja ya viwanja vyenye 'pitch' bora kabisa na ya kisasa ni Uwanja wa Benjamin Mkapa na gharama za ukarabati za uwekaji nyasi hizo mpya kwa mamilioni ya fedha, zilitolewa na SportPesa.

Kama hiyo haitoshi, moja ya viwanja vyenye vyumba bora vya kubadilishia nguo katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ni Uwanja wa huo na vyumba hivyo vilikarabatiwa na kutengenezwa na SportPesa. Nini kingine unakitaka kutoka kwa waungwana hawa, wanaojali kukua kwa michezo na maendeleo ya mchezo wa soka nchini?

Miaka minne, SportPesa wamefanikiwa kuandika rekodi kubwa ambazo wengine watahitaji miaka zaidi ya 10 kuifikia. Na inawezekana kabisa kama kutakuwa na msaada mkubwa wa watu kuendelea kuwaunga mkono, bila shaka watafanya makubwa maradufu katika maendeleo ya soka na michezo mingine hapa Tanzania.

## HABARI MICHEZO

# Harry Kane ataka ofa zipokelewe

**LONDON,** England

HARRY Kane amemwambia mmiliki wa timu hiyo, Daniel Levy apokee ofa ambazo zimekuwa zikimhitaji.

Klabu mbalimbali zimekuwa zikihitaji saini ya nyota huyo ili ziweze kupata huduma yake kwa ajili ya kuzitumikia kwa msimu ujao.

Miongoni mwa timu ambazo zimepeleka ofa ya kumpata nyota huyo ni pamoja na Manchester United ambayo iliweka dau la pauni milioni 90 kwa ajili ya kumpata mshambuliaji huyo.

"Hatima yangu itajulikana baada ya euro 2020, lakini kama kuna ofa Tottenham wanatakiwa kuipokea," alisema Kane akinukuliwa na BT Sport.

"Kwa sasa sitaki kuzungumza sana, lakini kama kuna ofa zitakuja zinatakiwa kupokelewa."

Imekuwa ikielezwa kuwa Kane amewaambia mabosi wake kwamba anataka kuondoka ndani ya Spurs ili kwenda kujiunga kwenye timu inayoshiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Kichapo cha mabao 3-1 walichokipata Spurs dhidi ya Leeds mwisho wa wiki kimepunguza matumaini kwa timu hiyo kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao na alijiunga na timu hiyo mwaka 2004.






# CAMAVINGA: SIJAAMUA HATIMA YANGU

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA Eduardo Camavinga ametoa taarifa mpya juu ya hatima yake na uwezekano wa kuondoka Rennes.

Nyota huyo raia wa Ufaransa, anajiandaa kuungana na kikosi cha Didier Deschamps kwa ajili ya michuano ya Ulaya mwezi ujao, huku taarifa juu ya uhamisho wake na wapi atakuwapo msimu ujao zikishika kasi.

Licha ya nyota huyo, kinda wa miaka 18 kuhusishwa na kuhamia mji mkuu wa Hispania kwa dau linalotajwa kuwa euro milioni 65, Camavinga anadai yeye kwa upande wake bado hajafikia hatua ya kufanya uamuzi kamili.

"Inafanya ujisikie vizuri sana kujua timu kama Real Madrid au Bayern zinavutiwa na hali yako," alisema Camavinga akiiambia France Football.

"Sitaweza kudanganya, bado sijaamua na familia yangu nini ambacho nitafanya."

Real Madrid walitajwa kuwa na mpango wa kutaka kumnasa kwa dau la euro milioni 75 msimu uliopita, lakini dau lake kwa sasa linaonekana kubadilika baada ya mazungumzo ya mkataba.

# *Juve yatishiwa kufukuzwa Italia*

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus wameonywa na Rais wa Shirikisho la Soka la Italia (FIGC), Gabriele Gravina kwamba wanakabiliwa na kufukuzwa kutoka Serie A kama hawatajiondoa katika Super League.

Klabu ambazo hazijajitoa kwenye ligi hiyo mpya ya klabu barani Ulaya ni Barcelona, Real Madrid na Juventus.

Miamba hao wa Italia, Real Madrid pamoja na Barcelona, ni moja ya matajiri watatu kati ya 12 wa Ulaya ambao walisaini kujiunga kwenye ligi hiyo yenye utata.

Milan, Inter na Atletico Madrid walijiondoa kwenye ligi hiyo muda mfupi baada ya kutangazwa mwezi uliopita, baada ya uongozi wa klabu kubwa sita za England kujiondoa, lakini Juve bado hawajayakataa mashindano hayo ambayo yanashinikiza mageuzi katika mpira wa miguu wa Ulaya.

UEFA wiki iliyopita ilizionya klabu hizo tatu kwamba zina hatari ya kuzuiliwa kwa sababu ya msimamo wao usioyumba.

Lakini, Juve ilitoa taarifa ya pamoja ikielezea maonyo hayo kama "hayavumiliki" na "hayakubaliki", ikisema kuwa mapinduzi ya muundo ni lazima yafanyike kwa faida ya mchezo.

Na Gravina ana matumaini Bianconeri watajiweka mbali na mashindano mapya yaliyopendekezwa, la sivyo watakabiliwa na kufukuzwa kwenye Ligi Kuu Italia.


"Sote tumechoka kidogo na vita hii ya vuta nikuvute kati ya Uefa na klabu hizi tatu. Natumai kuweza kupatanisha kati ya Juventus na Uefa.

"Sio nzuri kwa mpira wa miguu wa kimataifa, mpira wa miguu wa Italia, Juventus. Tayari tumesema kuwa chama cha mpira wa miguu kinaheshimu sheria.

Mwenyekiti wa Juventus, Andrea Agnelli ametajwa kuhusika kwa kuwa na jukumu katika kuandaa Super League.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED YAFANIKIWA KUMBAKISHA CAVANI

●●● Yampa mkataba mpya mwingine mshambuliaji huyo ambaye amekuwa msaada katika...

**MANCHESTER,** England

EDINSON Cavani amemaliza uvumi wa muda mrefu kwa kusaini mkataba mpya wa mwaka mmoja na Manchester United.

**Cavani alijiunga na United kama mchezaji huru Oktoba, mwaka jana na amefunga mabao 15 kwenye msimu wake wa kwanza nchini England.**

Straika huyo ambaye yupo kwenye kiwango cha kuvutia kwa sasa, mkataba wake wa awali na mashetani hao wekundu ulikuwa unamalizika mwishoni mwa mwezi ujao, lakini sasa atabakia hapo Old Trafford.

Cavani alionekana anaondoka baada ya baba yake, Luis kusema mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay hana furaha pale United na anataka kujiunga na Boca Juniors hapo Machi, mwaka huu.

Baada ya kufunga bao kwenye ushindi wa Jumapili wa 3-1 dhidi ya Aston Villa, kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer alidokeza kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 angependa ambakize hapo.

Cavani aliiambia tovuti ya klabu hiyo: "Kwa msimu mmoja nimekuwa na mapenzi mazuri na klabu hii kwa kila kitu kinachofanyika.

"Najihisi kuwa na mapenzi na klabu hii pamoja na wachezaji wenzangu hasa ninapokuwa nao kwenye vyumba vya kubadilishia nguo.

"Wamenipa hamasa kubwa kila siku na najua kwamba, kwa pamoja tunaweza kupata mafanikio makubwa.

"Tangu siku ya kwanza nilipowasili, nilijihisi kujiamini na imani ya kocha kwangu.

"Kama mchezaji imenipa hamasa na nguvu kubwa kupata nafasi ya kucheza soka hapa na nataka kuendelea kuwapo."

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMKATA SANCHO

WINGA wa Timu ya Taifa ya England na Borussia Dortmund, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21, sio kipaumbele cha usajili kwa klabu ya Manchester United. ***(Manchester Evening News)***

### CAMAVINGA ANUKIA ARSENAL

KIPAUMBELE cha usajili kwa Arsenal mwishoni mwa msimu huu ni kiungo, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 18, ambaye anachezea klabu ya Rennes. ***(Le10 Sport)***

### ZAKARIA SOKONI

KLABU ya Arsenal pia bado wana nia ya kumsajili kiungo wa klabu ya Borussia Monchengladbach na Uswisi, Denis Zakaria mwenye umri wa miaka 24. ***(90min)***

### GREALISH AGOMBEWA

MWAKILISHI wa kiungo wa Aston Villa na Timu ya Taifa ya England, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25, amesema kuna klabu nyingi ambazo zina mpango wa kumsajili nyota huyo. ***(SNTV via Birmingham Mail)***

### TOMORI MAMBO SAFI

KLABU ya AC Milan inataka kumsajili beki, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 23 kwa mkataba wa kudumu. Beki huyo wa kati kutoka England kwa sasa yupo Milan kwa mkopo akitokea Chelsea. ***(Goal)***

### BARCA NA HAALAND

NYOTA wa Burussia Dortmund, Erling Braut Haaland bado ndio kipaumbele cha usajili kwa Barcelona mwishoni mwa msimu huu.***(Marca)***

### AGUERO HATAKIWI

BARCELONA hawafikiri sana kuhusu usajili wa mshambuliaji wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Argentina, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32. ***(Mundo Deportivo)***

### SANCHEZ KUUZWA

KLABU ya Tottenham Hotspur inapanga kumuuza beki wa kati wa Colombia, Davinson Sanchez mwenye umri wa miaka 24, mwishoni mwa msimu. ***(Football Insider)***

### LEO, BELLERIN SOKONI

GOLIKIPA wa Ujerumani, Bernd Leno mwenye umri wa miaka 29 na beki wa kulia kutoka Hispania, Hector Bellerin (26), ni miongoni mwa wachezaji sita ambao Arsenal watawaingiza sokoni mwishoni mwa msimu. ***(Football London)***

### WILLOCK MAMBO SAFI

KLABU ya Newcastle United inataka kumsajili winga, Joe Willock mwenye umri wa miaka 21 kutoka Arsenal kwa mkataba wa kudumu. Willock amelivutia benchi la ufundi la Newcastle ambako anacheza kwa mkopo. ***(Talksport)***

HABARI MICHEZO

## Mgosi awaombea ruhusa wachezaji

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amewataka wazazi na walezi wote nchini kuwaruhusu mabinti zao ambao wana vipaji na uwezo wa kucheza soka ili kujiendeleza kwa sababu sasa hivi wanachangia kutunza familia kupitia mchezo huo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mgosi alisema ingawa si kwa kiasi kikubwa au kwa kila timu, lakini kwa sasa soka la wanawake limepiga hatua na tayari wadhamini wameshaanza kuliangalia kwa macho mawili.

Mgosi alisema katika timu ya Simba Queens, wachezaji wanalipwa mishahara na fedha hizo zinasaidia kutatua baadhi ya shida kwenye familia zao ikiwamo kukarabati au kujenga nyumba.

"Nitoe rai kwa wazazi na walezi wawaruhusu watoto au mabinti zao kwenda kufanya mazoezi na kucheza soka ili kuoyesha uwezo na vipaji vyao. Wanasaidia familia zao walikotoka, wamerekebisha nyumba, wengine wana mpango wa kununua magari, wamenunua viwanja, wamerekebisha mwonekano wa nyumba za familia zao, wanajitegemea wenyewe kwa sababu ya mpira tu," alisema Mgosi.

Aliongeza taratibu sasa soka la wanawake linaanza kuwa na faida kwa wachezaji, ingawa si kwa timu zote, lakini wazazi wanaweza kuwaruhusu mabinti zao japo wataanza kwenye mazingira magumu, lakini baadaye neema zitawafuata.

## Aweso amwaga jezi, vifaa Pangani

**Na Steven William,** PANGANI

MBUNGE wa Jimbo la Pangani ambaye ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amegawa jezi na vifaa mbalimbali kwa timu 16 zinazotarajiwa kushiriki Ligi Wilaya ya Pangani jijini Tanga, imefahamika.

Ligi hiyo itajulikana kwa jina la Aweso CUP na itaendeshwa chini ya usimamizi wa Chama cha Soka Wilaya, huku ikichezwa kwenye viwanja vya Sakura na Kumba.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa kwa timu hizo na Katibu wa Mbunge wa jimbo hilo, Salimini Selemani katika hafla fupi iliyofanyika katika ofisi za mbunge wao.

Akikabidhi vifaa hivyo, Selemani alisema lengo la kuanzisha ligi hiyo ni kuhakikisha Pangani inakuwa sehemu mojawapo ya kukuza na kuendeleza michezo kwa sababu inaamini ina vijana wenye vipaji.

Selemani alisema mbunge wao anaamini vifaa hivyo vitasaidia kuifanya ligi iwe na ushindani ambao utawapa burudani nzuri wananchi wa jimbo hilo.

# KISINDA KAMILI KUWAVAA NAMUNGO FC JUMAMOSI

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga chenye wachezaji 24 kinatarajia kuondoka jijini Dar es Salaam leo asubuhi na kuelekea Lindi kwa ajili ya kuwafuata wenyeji wao Namungo FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Majaliwa mjini Ruangwa.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mkurugenzi wa Mashindano ya Yanga, Thabiti Kandoro, alisema uamuzi wa kikosi chao kuondoka mapema unalenga kuwapa wachezaji muda mrefu wa kupumzika na kukamilisha maandalizi kuelekea mechi yao hiyo.**

Kandoro alisema katika msafara huo watakosekana wachezaji wawili ambao ni Balama Mapinduzi na Carlos Carlihnos ambao bado hawajawa fiti na wanabaki jijini kuendelea na matibabu chini ya uangalizi wa madaktari.

"Kwa taarifa nilizopokea kutoka kambini kikosi kinaendelea vizuri na miongoni mwa wachezaji 24 akiwamo Tuisila Kisinda ambaye alikuwa majeruhi, amerejea na yuko fiti kwa ajili ya mechi hiyo ijayo," alisema Kandoro.

Naye kocha mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na ana imani utakuwa mchezo wenye ushindani mkubwa kutokana na pande zote mbili kuhitaji kupata matokeo chanya ili kujiimarisha katika msimamo wa ligi.

Nabi alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali hivyo watashuka dimbani kupambana kusaka ushindi lakini wamewaheshimu wapinzani wote watakaokutana nao.

"Tumejiandaa vizuri kwa ajili ya michezo yetu yote ikiwamo dhidi ya Namungo FC, tunafanyia kazi mapungufu yetu na kujiimarisha kwenye safu ya ushambuliaji, viungo pamoja na mabeki ili kwenda kutafuta matokeo chanya katika mchezo huo," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema anafanya maandalizi ya mechi zote kwa uzito mkubwa kutokana na mahitaji ya kila mmoja wao kuhakikisha wanapambana kutafuta pointi tatu muhimu zitakazofanya watimize malengo yao ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

Yanga inashika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 57 huku vinara wa ligi hiyo wakiwa ni mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 61 wakati Mwadui FC ya mkoani Shinyanga inaburuza mkia ikiwa na pointi 19.

Msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21 unatarajiwa kumalizika ifikapo Julai 11, mwaka huu na Julai 18, mwaka huu itachezwa mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.




Washiriki wa kozi ya ukocha Ngazi ya Diploma D inayotambuliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), wakifuatilia mafunzo yanayoendeshwa kwa ushirikiano wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) na Taasisi ya Karibu Tanzania Organisation (KTO) hapa jijini Dar es Salaam. Kozi hiyo ni ya siku 10 na washiriki wanatoka katika wilaya mbalimbali hapa nchini. **PICHA: TFF**

# *Joana, Chiedza kumsindikiza Mwakinyo*

**Na Mwandishi Wetu**

MABONDIA wanawake kutoka Bulgaria na Zimbabwe watapamba ulingoni kabla ya pambano la kuwania ubingwa wa Afrika wa uzito wa Super Welter kati ya Mtanzania Hassan Mwakinyo dhidi ya Brendon Denes wa Zimbabwe litakalofanyika Mei 28, mwaka huu, kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Oysterbay jijini Dar es Salaam.

Joana Nwamerue wa Bulgaria ambaye hucheza kickboxing amethibitisha kuvaana na Chiedza Homakoma wa Zimbabwe maarufu kwa jina la The Queen Tiger.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Kelvin Twissa, alisema jana wameamua kuleta mabondia wa kigeni kuzichapa nchini kwa lengo la kuhamasisha maendeleo ya mchezo huo.

Twissa alisema mabondia hao wawili wana viwango vya juu anaamini ujio wao utawasaidia mabondia wa Tanzania kujifunza kitu kupitia kwao.

"Chiedza ni bondia namba moja Zimbabwe ambaye ameonyesha ukali wa hali ya juu mpaka kupachikwa jina la The Queen of Tiger. Tunatarajia kuwa na pambano la kusisimua siku hiyo mbali ya Mwakinyo na Denes," alisema Twissa.

Mapambano mengine siku hiyo yatakuwa ni kati ya Ibrahim Class dhidi ya Sibusiso Zingangwe wa Afrika Kusini wakati Shaaban Jongo atapigana na Olanrewaju Durodora kutoka Nigeria wakati Mbulgaria Pencho Tsvetkov atazichapa na Limbani Lano wa Malawi.

# Michezo

Jumatano Mei 12, 2021

Nipashe




United yafanikiwa kumbakisha Cavani UKURASA 22



Wachezaji wa Simba, Aishi Manula (kushoto), na Luis Miquissone baada ya kutua Johannesburg nchini Afrika Kusini jana kwa ajili ya mechi ya kwanza ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Kaizer Chiefs itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa FNB jijini humo. **PICHA: SIMBA**

## Gomes, Bocco watema cheche

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba waliwasili salama jijini Johannesburg nchini Afrika Kusini kwa ajili ya mechi ya robo fainali dhidi ya Kaizer Chief, wakiwa kwenye hali ya kujiamini.

Wakati Kocha Mkuu Didier Gomes akisema wanataka kuwafanya wanachama, mashabiki wa Simba na Watanzania wajivunie kuwa na kikosi hicho baada ya mechi, nahodha John Bocco amesema wana timu nzuri ya kupambana na timu yoyote ndani na nje ya nchi na wakiwa kwenye mazingira yoyote.

"Tuko tayari kucheza mechi hiyo. Tunajua mechi itakuwa ngumu. Tutacheza kwa kujituma kwa sababu tunataka kuwafanya wanachama, mashabiki wa Simba na Watanzania kwa ujumla kujivunia," alisema Gomes.

Nahodha Bocco alisema wamefanya maandalizi mazuri na mengine wanakwenda kuyamalizia huko Sauzi, hivyo anaamini mechi itakuwa nzuri kwa upande wao, ingawa wanajua Kaizer Chiefs ni timu ngumu na itakuwa na faida ya kucheza nyumbani.

"Mimi naamini hatujabahatisha kufika hapa. Klabu ilikuwa na malengo na sisi tulikuwa tunatimiza. Tunaamini tunakwenda kupata matokeo mazuri, ingawa tunajua mechi itakuwa ngumu na tutapata changamoto kubwa kwa sababu wenzetu watakuwa nyumbani, lakini wana timu nzuri pia," alisema nahodha huyo.

Kaizer Chiefs itaikaribisha Simba katika mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa FNB nchini humo.

# Simba, Yanga hazikwepani

## ●●● Zitakutana tena fainali FA endapo zitashinda mechi zao, serikali yawabeba mashabiki...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, Simba watawakaribisha Dodoma Jiji FC katika mechi ya hatua ya robo fainali ya michuano hiyo itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, wakati Yanga itawafuata Mwadui FC mkoani Shinyanga, imefahamika.

**Katika droo ya mashindano hayo iliyochezeshwa jana jijini inaonyesha robo fainali nyingine itakuwa ni kati ya Biashara United dhidi ya Namungo wakati Azam FC itaifuata Rhino inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza.**

Droo hiyo inaonyesha nusu fainali ya kwanza itawakutanisha mshindi kati ya Simba dhidi ya Dodoma au Rhino/ Azam FC na nusu fainali ya pili itakuwa ni kati ya Biashara United/Namungo FC au mshindi wa mchezo kati ya Mwadui FC dhidi Yanga.

Endapo Simba atatinga fainali atakutana na Yanga katika mechi ya fainali inayotarajiwa kuchezwa Julai 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Msimu uliopita, Simba ilicheza fainali na Namungo FC ya Lindi baada ya kuwafunga watani zao Yanga mabao 4-1 katika mechi ya hatua ya nusu fainali.

Meneja wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Baraka Kizuguto alisema baada ya droo hiyo mechi za hatua ya robo fainali zimepangwa kuchezwa kati ya Mei 25 hadi 27, mwaka huu.

"Nusu fainali hizo zitafanyika kwenye viwanja viwili, Ali Hassan Mwinyi, Tabora na Majimaji uliopo Songea, tunaomba wenyeji wa hivyo viwanja kuandaa na kuweka miundombinu mizuri kwa ajili ya michezo hiyo," alisema Kizunguto.

Naye Mkurugenzi wa Mashindano wa Simba, Khamisi Kisiwa, alisema wanatarajia mechi yao dhidi ya Dodoma jiji FC itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu ya ugumu wanapokutana na timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara pia.

Kisiwa alisema licha ya muda kwao kutokuwa rafiki kutokana na ratiba ya michuano ya kimataifa iliyopo mbele yao, lakini wamejipanga kuhakikisha wanatetea taji hilo la ubingwa wa Kombe la FA.

"Malengo yetu msimu huu ni kutetea ubingwa wetu ikiwamo wa Kombe la Azam Sports Federation Cup (Kombe la FA), kuhakikisha tunafanya vizuri katika mchezo wetu dhidi ya Dodoma Jiji FC, tunawafahamu, wamekuwa wakitusumbua mechi zote mbili za ligi msimu huu tulizocheza, kikubwa tutapambana kutafuta matokeo," alisema Kisiwa.

Naye Mkurugenzi wa Mashindano wa Yanga, Thabiti Kandoro, alisema wamejiandaa vizuri na wataenda Shinyanga kutafuta matokeo mazuri ili wasonge mbele katika mashindano hayo muhimu hapa nchini.

"Malengo yetu ni kushiriki michuano ya kimataifa, tunahitaji kupambana kutafuta matokeo mazuri katika michuano hiyo, hivyo tunahitaji kufanya vizuri katika mechi hiyo na kusonga mbele ili kufikia malengo yetu," alisema Kandoro.

Kiongozi huyo aliongeza katika dunia ya sasa katika mchezo wa soka hakuna mechi rahisi, hivyo watakiimarisha kikosi chao ili kusaka ushindi na si vinginevyo.

Wakati huo huo, taarifa iliyotolewa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa vyombo vya habari na kusainiwa na Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini, John Mapepele, imesema makubaliano yamefikiwa mechi hiyo ipangiwe tarehe nyingine ili kuwapa wapenzi wa soka kile walichokitarajia.

Mapepele alisema wizara imeliacha suala hilo la kupanga tarehe mpya kwa TFF na Bodi ya Ligi na kuwataka wakae haraka iwezekanavyo kutangaza mchezo huo utachezwa lini.

Pia Waziri Innocent Bashungwa ambaye alikuwa mwenyekiti wa kikao hicho, ameagiza pamoja na mashabiki hao wa zamani kurejeshewa tiketi na mfumo huo, pia uruhusu kuuzwa kwa tiketi zingine kupitia kwa mashabiki wapya, watakaoamua kuingia uwanjani siku hiyo hadi kufikia kamili ya watazamaji 60,000 wanaoruhusiwa kwa wakati mmoja.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >